**Hali** ya Maalim Seif yazidi kuimarika

UKURASA 2



**Ahukumiwa** kutokunywa pombe miezi 12 kisa kuua baba mkwe

UKURASA 5



**Aubameyang ampasua kichwa Arteta Arsenal**

UKURASA 20


# Nipashe

Jumanne Februari 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580479

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# JPM aombwa Katiba Mpya

• **Ni** katika Siku ya Sheria, yeye ataka kasi kesi za mabilioni benki... *Endelea ukurasa 2&3*





Baadhi ya Majaji wakimsikiliza Rais Dk. John Magufuli (hayupo pichani), alipokuwa akisoma hotuba yake katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini na Miaka 100 ya Mahakama Kuu jijini Dodoma, jana. **PICHA: IKULU**

## Serikali yafunguka chanjo ya corona

UKURASA 8

## Kodi za majengo, mabango zarejeshwa halmashauri

UKURASA 5


**MICHEZO** **GOMES SASA AITAKA SIMBA KULA VIPORO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# JPM ataka kasi hukumu kesi za mabilioni benki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli ameiagiza mahakama kutoa maamuzi ya haraka katika kesi zinazohusu biashara na mikopo ya benki kutokana na mabilioni ya fedha za benki kutolipwa na wadaiwa waliokimbilia mahakamani kufungua kesi.

Ameitaka mahakama kuliangalia suala hilo, huku akishauri kesi za namna hiyo zishughulikiwe mapema ili zisiathiri ukuaji wa uchumi.

Akizungumza jana kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Sheria na Miaka 100 ya Mahakama Kuu, Rais Magufuli alisema kuna ucheleweshaji wa mashauri hayo ikiwamo wateja wa benki waliokimbilia mahakamani kufungua kesi nyingi na kuweka mazuio ili kuchelewesha urejeshaji wa fedha wanayodaiwa na benki.

"Kesi hizi zipo nyingi na zingine zina zaidi ya miaka mitano na hapa nitoe mfano kwa kesi zilizofunguliwa mahakamani na wateja wakubwa wa benki, TPB, Azania na TIB," alisema.

Alibainisha kuwa kwa taarifa za Desemba 31, mwaka jana, Tanzania Bank Ltd ina kesi 36 zilizofunguliwa na wadaiwa wake zenye thamani ya Sh. bilioni 352.27, Benki ya Maendeleo (TIB) ina kesi 44 zenye thamani ya Sh. bilioni 167.2 na TPB ina kesi 16 zenye thamani ya Sh. bilioni 6.2 na CRDB kesi 282 zenye thamani ya Sh. bilioni 113.2.

"Katika benki nne wakati tuna benki 50 fedha ambazo zipo kule zimepakiwa ni Sh. bilioni 738.9, kwa hali hii ya wadaiwa kudaiwa na kukimbilia mahakamani na kuchelewa kutolewa maamuzi, ina athari nyingi kiuchumi, ni kupungua kwa uwezo wa benki zetu kutoa huduma kwa wateja," alisema.

Pia alisema athari nyingine ni kutopungua kwa gharama za riba na kusababisha kuongezeka kwa riba ili kufidia mikopo chechefu.

"Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kutokana na benki kulipa riba kwa amana zilizotumika kutoa mikopo kwa wateja wenye madeni waliokimbilia mahakamani na kesi zao kutotolewa maamuzi mapema," alisema.

Alisema athari nyingine ni kiasi kikubwa cha fedha kushikiliwa na wadaiwa sugu ambao wamefungua kesi mahakamani badala ya fedha hizo kutumika kutekeleza miradi mingine ambayo ingechochea uchumi.

"Napenda kutoa wito kwa mahakama kuliangalia suala hili vizuri kesi za namna hii zingefaa zishughulikiwe mapema ili zisiathiri ukuaji wa uchumi katika nchi yetu," alisema.

Alisema dhamira ya serikali haiwezi kutimia endapo kutakuwa na taasisi za kifedha husus̄an benki zenye ukwasi wa kutosha kutoa mikopo ya muda mrefu na riba nafuu kwa wananchi.

"Mahakama ijipange kushughulikia changamoto hiyo niliyoeleza kwa kuwa inachelewesha ukuaji wa uchumi, niwaombe wasajili wafuate sheria hasa kwenye kesi ambazo haziwezi kufunguliwa... kesi zinazohusu kodi na biashara, kuna wafanyabiashara kazi yao ni kupaki kesi, hili suala ni la kushughulikia," alisema.

**MAFANIKIO**

Alisema tangu mwaka 2016 alivyoingia madarakani serikali ilisaini mkataba wa mkopo kutoka Benki ya Dunia ya Dola za Marekani milioni 65 sawa na Sh. bilioni 135 na kila mwaka serikali imekuwa ikitenga fedha na kuhakikisha zinatolewa na zimesaidia maboresho makubwa kwenye mahakama.

Alisema miaka mitano iliyopita zimejengwa Mahakama Kuu za Kanda tatu, Mahakama za Hakimu Mkazi tano, wilaya 15, mahakama za mwanzo 18 na mahakama ya kutembea.

"Tumeanzisha mahakama ya kutembea yaani (mobile court) ambapo mwaka 2020, imesikiliza mashauri 778, tumeimarisha mifumo ya TEHAMA, ikiwamo mfumo wa kielektroniki ya kusajili mahakama," alisema.

Aidha, alisema kwa miaka mitano iliyopita serikali ilianzisha Mahakama Kuu kitengo cha uhujumu uchumi.

"Tuna jumla ya majaji 88, najua bado Jaji Mkuu majaji hawajatosha na ombi umeniletea nafanyia kazi kikamilifu, pia kuna mahakimu 1,287," alisema.

Kuhusu watumishi 200 alioahidi, Magufuli alisema "Wale wahusika wote washughulikie hili suala ili likamilike mapema kwasababu ahadi ni deni nisije nikapelekwa mahakamani kwa uongo, kwa hiyo Wizara ya Utumishi ilisimamie hili haraka sana."

Rais Magufuli alisema hatua hizo zimesaidia kuisogeza mahakama kwa wananchi na kuboresha huduma zake ambapo kwa miaka ya hivi karibuni kasi ya kusikiliza kesi imeongezekana na kupunguza mrundikano wa kesi.

"Mwaka 2020, Mahakama za Mwanzo zilisikiliza mashauri 164,758, Mahakama za Wilaya zilisikiliza mashauri 43,149 ambapo mashauri yenye zaidi ya miezi miwili yalikuwa asilimia 18, Mahakama Kuu divisheni ya Uhujumu Uchumi ilisajili mashauri 11 na kusikiliza mashauri 9, Mahakama ya Rufani ilisikiliza mashauri 1,216,"alisema.

Alisema hayo ni mafanikio makubwa na kwamba imechangiwa na maboresho yaliyofanyika kwenye taasisi nyingine zinazosimamia masuala ya haki na sheria nchini ikiwamo kutenganishwa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwendesha Mashataka wa Serikali na kuanzisha Ofisi ya Wakili Mkuu.

"Kasi ya upelelezi na uchunguzi imeongezeka, kasi ya usikilizaji mashauri kwa mahakimu imeongezeka na kurahisisha upatikanaji wa haki," alisema.

Kadhalika, alisema magereza yaliyopo uwezo wake wa kuchukua wafungwa na mahabusu ni 29,902 lakini waliopo hivi sasa kwenye magereza ni 33,000.

**AMPANDISHA CHEO JAJI**

Alimpandisha cheo Jaji Zephrine Galeba wa Mahakama Kuu, Kanda ya Musoma kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani kwa ushujaa wake wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye kutoa hukumu kwenye kesi ya Mgodi wa North Mara dhidi ya Gerald Zumbi.

"Wakati umefika wa kuweka mikakati itakayofanya lugha ya Kiswahili kutumika kwenye mahakama ngazi zote, Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa duniani, sioni sababu Mahakama kwanini hamtaki kutumia Kiswahili, kushindwa kutumia lugha hii sio kwamba tunawanyima haki wananchi bali pia kuwaongezea gharama ya kutafsiri kesi," alisema.

Hata hivyo alisema ombi la Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma la kuomba majaji aliahidi kuliangalia.

**WALIOMBEZA KWA KISWAHILI**

Aliwaomba Watanzania katika matumizi ya Kiswahili wasione aibu.

"Mimi nilipoingia madarakani nilianza kutoa hotuba kwa Kiswahili nikaambiwa sijui Kiingereza wala sikujali, kana kwamba kujua Kiingereza ndio kujua kusoma, inawezekana hata huyu Jaji ataambiwa hajui Kiingereza," alisema.

Alisema matumizi ya lugha ya Kiswahili itasaidia wananchi kujua ukweli wa hukumu zao na kuzitaka mamlaka zinazohusika zitafsiri sheria zilizopo na kutunga kwa Kiswahili.

Alipongeza Mahakama kwa kutimiza miaka 100 tangu kuanzishwa kwake na kwamba imekuwa na mchango mkubwa kwa Taifa kwenye maendeleo na ustawi wa nchi kwa kusimamia haki, kulinda amani na uhuru.




Mkurugenzi Mtendaji wa TRC, Masanja Kadogosa, akiteta na mmoja wa wafanyabiashara katika hafla iliyoratibiwa na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) na kudhaminiwa na Benki ya NBC kwa dhumuni la kukutanisha wadau wa sekta binafsi, Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Shirika la Ujenzi la Uhandisi la China (CCECC), kujadili ushiriki wa sekta binafsi katika kufanikisha na kukamilisha mradi wa SGR kutokea Mwanza- Isaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU** .

## Afya ya Maalim Seif yaimarika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, bado anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, na hali yake ya afya inaimarika.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema Maalim Seif bado yupo hospitali akiendelea kupatiwa matibabu baada ya kulazwa tokea Ijumaa.

"Maalim Seif yupo vizuri, hivyo niwaombe wananchi na wafuasi wa ACT- Wazalendo wasiwe na wasiwasi, afya yake imeimarika," alisema Mazuri.

Aidha, alisema mke wa kiongozi huyo, Mama Awawena naye hali yake ipo vizuri na yupo nyumbani kwake Mbweni akiendelea na matibabu.

Mkurugenzi Kinga wa Wizara ya Afya, Dk. Fadhil Muhammed, alisema ni kweli Maalim Seif yupo Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo alifikishwa kwa ajili ya kupatiwa matibabu kama wagonjwa wengine.

"Maradhi yanayomsumbua Maalim Seif mimi sijui, ninachokijua ni kweli amelazwa Hospitali ya Mnazi Mmoja," alisema."Vile vile tumeendelea kupokea viongozi mbalimbali wa kimataifa wakiwamo Rais wa Msumbiji, Rais wa Ethiopia na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China,"alibainisha Dk, Abbasi

Alisema ziara hizo ni kielelezo cha kuimarika uhusiano na ushirikiano wa Tanzania na nchi mbalimbali duniani.

## HABARI KITAIFA

# Mahakama yakabiliwa uhaba watumishi 4,728

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Mahakama nchini, Prof. Ibrahim Juma, amesema mahakama inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi 4,728 hali inayoathiri utendaji wake katika upokeaji na usikilizaji mashauri.

Kutokana na hali hiyo, amewasilisha ombi kwa Rais John Magufuli kuongezewa watumishi hao wa kada mbalimbali ikiwamo mahakimu na majaji.

Prof. Juma aliyasema hayo jana kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Sheria na Miaka 100 ya Mahakama yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema mahitaji halisi ya watumishi ni 10,351 hadi kufikia Desemba 2020 Mahakama ilikuwa na watumishi 5,623 huku upungufu ukiwa ni watumishi 4,728 sawa na asilimia 46.

"Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa takwimu hizi upungufu huu unaathiri utendaji kazi wetu hasa eneo la jukumu kuu la kupokea na kusikiliza mashauri," alisema.

Alitolea mfano kuwa Mahakama ya Rufani inakabiliwa na wingi wa mashauri yanayofika takribani 1,100 kwa kila jopo moja la majaji watatu ambao uwezo wake ni wastani wa mashauri 200 kwa mwaka.

"Uwezo wa Jaji mmoja wa Mahakama Kuu kwa mwaka ni kusikiliza mashauri 220 na hakimu ngazi ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ni mashauri 250, hata hivyo hali ilivyo sasa Jaji mmoja ana wastani wa mashauri 491 na hakimu wastani wa mashauri 273," alisema.

Kuhusu miundombinu, jaji huyo alisema mwaka huu wa fedha wameanza mchakato wa ujenzi wa Mahakama za Wilaya 33 ili kufikia dhamira ya kuwa na mahakama kila wilaya ili wananchi wasitembee umbali mrefu kuzitafuta haki.

Hata hivyo, alisema bajeti inayotolewa ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya ofisi zinazohudumiwa nchini ikiwamo watumishi na vitendea kazi.

Awali, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika(TLS), Dk. Rugemeleza Nshala, alisema mawakili wameshuhudia ucheleweshaji wa kesi na kuahirishwa kwa kisingizio cha kutokamilika kwa upelelezi na mahakama chakavu.

"Nililalamika mwaka jana kuhusu ucheleweshaji wa kesi za jinai kwa kisingizio cha kutokamilika upelelezi, hali haijabadilika mahabusu wengi bado wanaendelea kusota magerezani kwa kisingizio cha kutokamilika upelelezi, hii si sawa hata kidogo, napenda kusema hapa ukimshika mtu na kuendelea kumuweka ndani huna uwezo wa kufidia muda wa uhuru uliomnyang'anya, makosa yote yadhaminike," alisema.

Alisema inapaswa anapokamatwa mtu upelelezi ukamilike na kama haujakamilika apewe dhamana hivyo makosa yadhaminiwe.



Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Venance Msafiri (kushoto), akimkabidhi cheti cha usajili wa Chama cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima wa Ngano Nangwa (UWANA), Mwenyekiti wa Chama hicho, Clement Fissoo (kulia). **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Lipumba amkumbusha Magufuli Katiba Mpya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amemwomba Rais John Magufuli kukamilisha kiporo cha upatikanaji wa Katiba Mpya kama alivyoahidi.

Lipumba alitoa ombi hilo jana, katika Maadhimisho ya Wiki ya Sheria na Miaka 100 ya Mahakama Kuu baada ya kupewa nafasi na Rais Magufuli ya kusalimia hadhara iliyokuwapo.

Mwenyekiti huyo alisema katika hotuba ya Rais aliyoitoa Novemba 2015, aliwaeleza wabunge kuwa katika uongozi wake atahakikisha yale aliyoahidi yanatekelezwa ikiwamo kiporo kilichoachwa cha kukamilisha Katiba.

"Watanzania wengi walishiriki kutoa maoni ili ipatikane Katiba Mpya, ukasema umelipokea na utalitekeleza lakini ulipokuwa ukipokea ripoti ya Tume ya Uchaguzi (NEC) 2016, ulisema masuala ya Katiba iliyopendekezwa na ukasema kama kuna watu wana maoni mengine serikali yako ipo wazi itapokea," alisema.

Alieleza kuwa viporo ambavyo hakutekeleza miaka mitano iliyopita avitekeleze katika miaka mitano yake ya sasa.

"Nakuombea kwa dhati Mwenyezi Mungu akupe nguvu hivi viporo vyote katika kipindi hiki, uweze kuvitekeleza unapomaliza kipindi chako watu watakaoweza kulinda mafanikio ni kuwa na Katiba inayotokana na mapendekezo ya wananchi wa Tanzania," alisema.

Lipumba alitoa wito kwa Rais ambaye alikuwa mjumbe wa Bunge Maalum la Katiba na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge hilo.

"Unazungukwa na watu wazito waliokuwapo kwenye mchakato kama Prof. Palamagamba Kabudi, kuna wajumbe wa Tume ya Jaji Warioba, kuna vijana wako, Humphrey Polepole, umezungukwa na wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba, ukihitaji vitendea vipo vya kutosha, Naibu Spika pia aliongoza upande wa vyuo vikuu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema ana uhakika Rais atashughulikia suala hilo, na kuwa na Katiba inayotokana na maoni ya wananchi.

Kwa upande wake, Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mtungi, alishauri vyama vya siasa mwaka 2021 kuwa wazalendo na kuacha masuala ya kususa vikao vya bunge.


VisionFund TANZANIA

## MASAHIHISHO

**Katika gazeti letu la Nipashe toleo na. 0580475 la tarehe 29.1.2021, ukurasa wa 23, tulitumia nembo isiyo sahihi ya VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED katika tangazo la Taarifa za Fedha. Nembo sahihi ni kama ilivyoonekana hapo juu. Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI No: 224 YA 2020**

**ACCESS BANK TANZANIA LTD ............................................ MDAI**

**DHIDI YA**

**VUMILIA ANDREA MAKERE @ VUMILIA ANDREA SWAI............MDAIWA**
**CRDB BANK PLC ............................................................ MDAIWA**

**Kwa**
**VUMILIA ANDREA MAKERE @ VUMILIA ANDREA SWAI**
**DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Jumatano, Tarehe 03 Mwezi 02 Mwaka 2021 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIZO:**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 29 mwezi wa 01 mwaka 2021**

**Hakimu Mkazi**
**Mahakama Ya Wilaya**
**Kinondoni**

RIPOTI MAALUM -2

# Madhila yanayokumba wagonjwa hospitalini



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Hamis Mkaruka, akitizama sinki lililopo Kituo cha Afya Nyangoto Kata ya Matongo, Nyamongo, ambalo limetelekezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja, lililokuwa lanatumika kwa ajili ya kufulia nguo za wagonjwa wakiwamo kinamama wanaojifungua, lakini kwa sasa halitumiki kwa madai limeziba. **PICHA: DINNA MANINGO.**

**Na Dinna Maningo, TARIME**

SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilibainisha kero zinazowakabili wagonjwa wanaofika kwenye Kituo cha Afya Nyangoto wilayani Tarime mkoani Mara. Endelea na sehemu mwisho ya udadisi huu wa Nipashe kujua mustakabali wake...

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Nyangoto, Josephat Kirambo, alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 1987 na kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, kinahudumia wakazi 30,110 kutoka kata mbili za Matongo na Kemambo zenye vijiji vinane.

Kirambo alisema kuwa mbali na huduma kwa vijiji hivyo, kituo hicho pia kinatoa huduma kwa wakazi wa vijiji jirani vinne ambavyo ni Nyakunguru, Nyarwana, Nkerege na Weigita vya Kata ya Kibasuka.

Pia, kinahudumia wakazi wa Kata ya Nyarukoba wanaotoa vijiji vya Msege, Genkuru, Komarera, Nyabirongo na wilaya ya jirani ya Serengeti ambao vijiji vya Nyiboko, Borega, Nyamitita na Nyansurura vinakitegemea kituo hicho kwa matibabu.

Mganga huyo alisema kituo hicho kina watoa huduma ya afya 38 na sasa kinakabiliwa na tatizo la upungufu wa dawa, watumishi na ukosefu wa duka la dawa la kituo.

Kuhusu kinamama wanaojifungua kuondoka na nguo kwenda kufua nyumbani, mganga huyo alisema: "Ile sehemu ya kufulia nguo, maji machafu yaliziba, watu walikuwa wanaweka nepi na vitambaa wanashindilia mle ndani ya tundu la kwenye sinki.

"Tulielekeza namna ya kufanya usafi wakati tunaandaa sehemu nyingine na wakati mwingine nilikuwa ninasimamia mimi mwenyewe, lakini hawakuelewa.

"Tulielekeza kama unafua nguo za uzazi zenye damu nyingi, kusanya zile damu pamoja ziwekwe kwenye shimo la pracenta, lakini haikuwezekana, siamini kama mtu aliambiwa akafulie nyumbani kama yupo, aliyewaambia kwa kweli alifanya makosa.

"Tunaomba mtusamehe, halitajirudia tena na sina taarifa ya mtu kuambiwa aondoke na kondo, hakuna aliyenilalamikia," alisema mganga huyo kwa unyenyekevu mbele ya viongozi hao.

Hata hivyo, Bhoke Marwa, Mkazi wa Kijiji cha Matongo, Kata ya Matongo, alibainisha kuwa Septemba mwaka jana alijifungua kituoni hapo na aliambiwa na muuguzi ambaye hajui jina lake kuwa aondoke na nguo zake kwenda kufua nyumbani.

**WAGONJWA WALIPIA VITANDA**

Mganga Mfawidhi huyo alikiri wagonjwa kutozwa Sh. 5,000 kwa ajili ya kitanda, Sh. 2,000 za vipimo na Sh. 5,000 ya usajili, akifafanua:

"Wanachangia Sh. 5,000 ya usajili wa mgonjwa, vipimo Sh. 2,000 kwa kila kipimo na Sh. 5,000 ya kitanda, huu ni utaratibu mpya tulioelekezwa baada ya kuwapo kwa upungufu wa dawa.

"Tulipewa maagizo na halmashauri na sisi ni kusimamia na malipo yote yanapitia kwenye mfumo."

Alisema kuwa kituo hicho hakipati dawa kwa kuwa kilikuwa kinadaiwa deni Sh. milioni 82 na kwamba kupitia mapato hayo ya ndani, kimefanikiwa kulipa Sh. milioni 27 na kubaki na deni la Sh. milioni 55.

Tabibu huyo alibainisha kuwa uamuzi huo wa kuwatoza fedha wagonjwa umesababisha kutokuwapo uhusiano mzuri kati ya wataalamu wa afya kituoni hapo na wateja wao (wagonjwa) hasa pale kunapotokea mgonjwa amekosa dawa na huduma amelipia.

**DED ALONGA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Tindwa, alisema upungufu wa dawa haupo kwenye kitjuo hicho pekee, bali ni tatizo katika zahanati na vituo vyote vya afya katika eneo lake hilo la kazi.

Alisema halmashauri inadaiwa na MSD Sh. milioni 185 na wanajitahidi kuhakikisha deni hilo linalipwa, ili wananchi wapatae huduma bora.

"Zahanati ya Kerende itapandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya, Zahanati ya Itandora inaelekea kukamilika na Genguru ili kupunguza wimbi la wagonjwa katika Kituo cha Afya Nyangoto.

"Tuna changamoto ya gari la wagonjwa kwenye vituo, tuna gari moja la Kituo cha Nyangoto linalolazimika kutoa huduma kwenye vituo vingine," Tindwa alifafanua.

MAAGIZO YA WAITARA

Baada ya kusikiliza maelezo ya wananchi na viongozi wa kituo hicho pamoja na halmashauri, Waitara alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo kuhakikisha yanafanyika mabadiliko makubwa ya usimamizi wa huduma ya afya katika wilaya hiyo, kikiwamo Kituo cha Afya Nyangoto.

Alisema mabadiliko hayo yatasaidia kuondoa malalamiko mengi ya wananchi ambao wengi wao wanaopata huduma kwenye vituo vya serikali, ni wenye uwezo wa chini kimapato.

Waitara alisema wananchi wasipopata huduma vizuri, huisema vibaya serikali na chama, jambo ambalo halimpendezi kwa kuwa kazi yake ni kuhakikisha anatatua kero zinazowakabili wananchi.

## HABARI KITAIFA

# Halmashauri zarejeshewa kodi za majengo, ushuru wa mabango

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kurudisha ukusanyaji mapato ya kodi ya majengo na ushuru wa mabango kwa halmashauri nchini, huku ikiwataka Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia ukusanyaji wa vyanzo hivyo.

Julai 2016, serikali ilihamisha vyanzo hivyo Serikali Kuu ambapo mapato yake yalikuwa yakikusanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Akizunguma jana na waandishi wa habari kuhusu hatua hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alisema hatua hiyo ni mkakati wa serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

"Kwa lengo la kuimarisha jinsi gani tutakusanya kodi na kuweza kuwafikia wenye majengo, serikali imekuja na maelekezo kwamba kuanzia sasa utaratibu wa kodi za majengo utasimamiwa na mamlaka za serikali za mitaa katika halmashauri zetu na manispaa zetu," alisema.

Alisema wakurugenzi wa halmashauri zote nchini 185 watahusika na kusimamia ukusanyaji wa kodi za majengo.

"Zoezi hili litaanza mara moja, wakurugenzi wote tunawaelekeza sasa kodi za majengo wataenda kuzisimamia na kuhakikisha majengo yote yanalipiwa kodi, mamlaka hizi zina uwanja mpana wa kuwafikia watu wote wenye majengo," alisema.

Aliwaagiza wakurugenzi kuhakikisha wanawatumia wale maofisa biashara, watendaji wa kata, mitaa na vijiji na kuhakikisha majengo yote yanapiliwa kodi.

Hata hivyo, alisema maelekezo mengine ya kiutendaji kwa wakurugenzi hao kwenye ukusanyaji wa vyanzo hivyo yatatolewa.

Kuhusu, ushuru wa mabango, Jafo alisema: "Tunawaelekeza wakurugenzi kuanzia sasa ukiachia yale maeneo yanayokusanywa na TARURA na TANROAD, lakini yale maeneo yote ambayo TRA ilikuwa inakusanya ushuru wa mabango sasa wakurugenzi watakuwa wanakusanya ushuru wote wa mabango."

Aliongeza "Wakurugenzi wanafahamu kila aina ya bango lipo wapi na biashara gani ya bango inaendelea ,eneo hili tunataka tuone ufanisi wa hali ya juu katika ukusanyaji wa mapato lengo letu ni kupata fedha kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania."

**VITAMBULISHO VYA WAMACHINGA TAYARI**

Kadhalika, Waziri Jafo alisema vitambulisho vya wajasiriamali vya mwaka 2021, vipo tayari na vimeshambazwa mikoani katika ofisi za wakuu wa mikoa.

"Kuanzia sasa vitakuwa chini ya wakuu wa mikoa na watashusha katika mamlaka ya serikali za mitaa, katika eneo hilo wakurugenzi watasimamia zoezi zima la ukusanyaji wa uuzaji wa vitambulisho hivyo na tunataka tuone jinsi gani wakurugenzi wa halmashauri wamejikita katika kufanya vizuri," alisema.

Alieleza vitambulisho hivyo vitauzwa kwa gharama ile ile ya awali Sh. 20,000 ili mjasiriamali afanye biashara zake mwaka mzima.

# Ahukumiwa kutokunywa pombe miezi 12 kisa kuua baba mkwe

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma imemwachia huru Boniphace Kachila, mkazi wa Kijiji cha Kiyungwe Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma kwa sharti la kutokunywa pombe kwa miezi 12 na kutokufanya kosa lolote baada ya kutiwa hatiani kumuua baba mkwe bila kukusudia.

Kesi ya mauaji ya bila kukusudia namba mbili ya mwaka 2021 kosa linalotajwa kutendeka Juni 13, mwaka 2019, inaelezwa mshtakiwa akiwa na marehemu baada ya kutoka kibaruani walipita kwenye kilabu cha pombe kunywa wote wakiwa wamelewa, waliondoka kurejea nyumbani na wakiwa njiani uliibuka ugomvi kati yao uliosababisha kifo cha Donansiano.

Wakili wa serikali Clement Masua, alidai mshtakiwa baada ya kutenda kosa hilo alijaribu kukimbia na baadaye kurudi baada ya kukutana na wake wa marehemu, na kuwapeleka eneo la tukio na kumkuta baba mkwe akiwa kwenye hatua za mwisho za kukata roho.

Alieleza uchunguzi wa daktari ulionyesha marehemu alipoteza maisha baada ya fuvu kupasuka na damu kuvuja kwani katika ugomvi huo inaelezwa marehemu alipigwa ngumi na mateke sehemu mbalimbali za mwili.

Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Jaji Athumani Matuma, alisema kwa kuzingatia pande zote mbili na mazingira ya kosa ni wazi mshtakiwa anahitaji huruma ya mahakama mshtakiwa amekuwa muungwana tangu hatua za awali kukubali kosa.

"Hakuna mahali popote kwenye mwenendo wa shauri panapo onyesha kuna upelelezi ulifanyika ili kumbaini aliyetenda kosa wakati ugomvi huo unatokea hakuna aliye kuwapo, hivyo mshtakiwa angeweza kudanganya... huu ni uungwana mkubwa katika utoaji wa haki.

Jaji Matuma alisema mahakama hiyo inamwachia huru mshtakiwa kwa sharti la kutokufanya kosa lolote katika kipindi cha miezi 12 ikiwamo sharti la kutokunywa pombe kwa kipindi hicho cha uangalizi na endapo atavunja sharti lolote atarudishwa mahakamani mbele yake kuhukumiwa kwenda jela.

WOMEN FUND TANZANIA-TRUST
Empowering Local Women Heroes

**BODI YA WADHAMINI WOMEN FUND TANZANIA (WFT-TRUST)**

**WITO KWA MAPENDEKEZO YA KUENDELEZA HAKI ZA WANAWAKE, WASICHANA NA HAKI ZA WATOTO TANZANIA KWA 2021**

Bodi ya Wadhamini ya Women Fund Tanzania (WFT-Trust) ni mfuko wa uwezeshaji wa haki za wanawake ambao ulisajiliwa mnamo Septemba 2008 kama shirika lisilo la kiserikali na kubadilishwa kuwa Mfuko wa Dhamana mnamo Septemba 2019. Mfuko huo unaongozwa na maono ya kufikiwa kwa jamii yenye usawa na haki ambapo wanawake, wasichana, na watoto wanashiriki kikamilifu katika mabadiliko chanya ya jamii zao. Mfuko unatoa ufadhili ili kutekeleza hatua mbalimbali zinazolenga katika kujenga na kuimarisha vuguvugu la kiharakati la ujenzi wa TAPO la wanawake na wasichana hapa nchini na harakati za utetezi wa haki za wanawake, wasichana, na watoto kwa ujumla wake. Mfuko unadhamiria kufikia makundi yote ya kijamii ikiwa ni pamoja na walio pembezoni kwa msingi wa umri, jinsia, tabaka, uwezo, rangi, n.k. Mwaka huu, Mfuko wa Dhamana wa WFT-Trust utatoa kipaumbele katika kutekeleza miradi ambayo itashughulikia makundi ya utetezi wa haki za wanawake, wasichana, na watoto katika maeneo yaliyoainishwa hapo chini.

WFT-Trust inakaribisha maombi kutoka kwa mashirika ya haki za wanawake, wasichana, na watoto yaliyosajiliwa kisheria, mashirika ya jamii, vikundi, pamoja na taasisi zinazofanya kazi katika moja au zaidi ya maeneo yafuatayo:

1. Ukatili dhidi ya Wanawake, Wasichana, na Watoto - ukilenga kushughulikia rushwa ya ngono, unyanyasaji unaoathiri afya hususan afya ya akili kwa wanawake, wasichana, watoto na vikundi vingine vya kijamii wakiwemo wafanyakazi wa nyumbani wa kike na wale walioathiriwa na mila/tamaduni kandamzi katika jamii za vijijini na mijini.
2. Uongozi wa Wanawake na Ushiriki wa Kisiasa katika kipindi cha baada ya uchaguzi - Nyanja hii inalenga kushughulikia maeneo mbalimbali katika muktadha wa ushiriki mpana wa wanawake na wasichana katika uongozi na siasa katika kipindi cha baada ya uchaguzi mkuu na haswa katika kuangalia masuala yanayoibuka ambayo yanazuia wanawake na wasichana kushiriki kikamilifu katika michakato ya baada ya uchaguzi ikiwa ni pamoja na mifumo na taratibu zenye changamoto ambayo inawazuia wanawake na wasichana kuingia na kukaa katika nafasi za uongozi katika jamii zao, katika sekta binafsi, na nafasi nyingine za uongozi.
3. Haki ya Uchumi Endelevu - Utekelezaji wa shughuli mbalimbali zenye lengo la kuvunja vizuizi ambavyo vinapunguza ushiriki wa wanawake na wasichana katika shughuli za kiuchumi na vinavyokwamisha wanawake kufaidika na fursa mbalimbali katika sekta tofauti ikiwemo uchimbaji wa madini, usafirishaji wa bidhaa nje n.k.
4. Haki ya Mazingira - Maombi kwa ajili ya utekelezaji kushughulikia changamoto zinazowakabili wanawake wanaofanya kazi au wanaoathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa, ukataji miti, na kuhakikisha ushiriki sawa katika maendeleo, na katika utekelezaji wa sharia, kanuni, na sera za mazingira.
5. Haki ya Elimu - Kutekeleza shughuli mbalimbali katika muktadha wa kuhakikisha kufikiwa kwa haki ya elimu kwa wasichana, kuboresha uelewa wa jamii kuhusu haki za elimu za mtoto wa kike, kuimarisha ushiriki wa jamii katika usimamizi wa haki ya elimu kwa wasichana, kuvunja mila potofu na kupinga vitendo vya kikatili dhidi ya wasichana katika muktadha wa haki ya elimu kama ubakaji, mimba za utotoni, ndoa za utotoni, na rushwa ya ngono.
6. Utafiti, Uhifadhi Taarifa, na Ushirikishwaji wa Vyombo vya Habari - Kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga katika kuibua tafiti mbalimbali, uhifadhi wa taarifa, kuhamasisha matumizi chanya ya vyombo na mifumo ya habari na upashanaji habari kwa lengo la kuibua mijadala, kuhifadhi, kuimarisha utetezi na kujenga utamaduni wa kuenzi michango na ushiriki wa wanawake katika ujenzi wa Taifa letu katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kiutamaduni. Kubadilisha mapokeo hasi kuhusu wanawake na wasichana na kujenga utambuzi mpana wa michango mipana ya wanawake na wasichana kupitia hadithi, simulizi, machapisho na nyaraka.
7. Michezo, sanaa na utamaduni - Kutekeleza shughuli mbalimbali za zinazolenga kushughulikia changamoto za mazoea ya kutengwa, upendeleo wa kitamaduni na kanuni za kijamii katika michezo, sanaa maarufu na utamaduni ikiwa ni pamoja na kupinga matumizi ya lugha zinazodhalilisha na kuondoa utu na staha ya mwanamke na msichana katika jamiii.
8. Kushughulikia changamoto na maswala yanayowakabili wahamiaji - kwa kuzingatia kulinda utu wao na haki za wanawake na watoto
9. Masuala Haki ya Afya ya Uzazi - Kukuza uelewa wa masuala mtambuka na haki ya afya ya uzazi kwa wanawake na hatua za kusaidia harakati za utetezi unaojikita katika haki na wajibu katika kushughulikia maswala yanayowanyima wanawake na wasichana kufanya maamuzi, uwezo wa kuamua na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa marika sahihi kuhusu mabadiliko ya kimwili,upatikanaji wa huduma na umuhimu wa kujipanga ili kufikia malengo yao.
10. Kujenga vuguvugu la kiharakati la kuleta pamoja wanawake na wasichana kimkakati na kuimarisha TAPO la wanawake Tanzania - Kutekeleza shughuli mbalimbali za kukuza njia za makutano katika kuharakisha mabadiliko ya ndani ya harakati za wanawake na harakati zingine za kijamii pamoja na zile zinazofanya kazi kuendeleza haki za walemavu, haki za watoto, haki za afya ya uzazi, haki za wahamiaji na haki ya mazingira kwa hatua za pamoja na utekelezaji wa pamoja. Kuimarisha harakati za kubadilisha mifumo,sera na mitizamo ya kijinsia katika tamaduni, kanuni za kijamii, na pia katika mifumo ya sera na sheria katika viwango tofauti

Tunatoa Ruzuku kwa Kupitia Madirisha Yafuatayo:

**1. DIRISHA DOGO LA UFADHILI**

Dirisha hili ni kwa ajili ya asasi na mashirika ya kijamii ya kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto, na vikundi vya wanaharakati vilivyosajiliwa walio katika maeneo ya vijijini na mijini. Dirisha hili linafunguliwa pia kwa vikundi vya jamii yanayoanza, na yenye nia ya kujenga uwezo wao wa kiundeshaji na wa kukuza uhamasishaji unaopelekea kukuza haki za wanawake, wasichana na watoto katika jamii zao.

Waombaji wanaostahili kuomba ruzuku chini ya dirisha hili wanahitaji kuzingatia yafuatayo:

- Muda wa utekelezaji/mradi wa kutekelezwa kati ya miezi 0 hadi 3
- Shughuli za mradi zenye makusudio ya kuibua/kutoa sauti kuhusu maswala ya wanawake, wasichana na watoto, pamoja na wale waliotengwa na walio katika mazingira magumu katika jamii
- Waombaji wa mara ya kwanza kutoka katika vikundi vya jamii.

**2. DIRISHA LA KATI LA UFADHILI**

Waombaji wanaostahili kuomba ruzuku chini ya dirisha hili wanahitaji kuzingatia yafuatayo:

- Pendekezo la mradi chini ya dirisha hili linapaswa kuzingatia hatua za kusaidia wanawake, wasichana kwa kupitia mashirika na vikundi vyao kukuza haki za wanawake, wasichana na watoto kwa njia ya kujenga/kuimarisha uwezo halisi wa dhana na shirika, utaalamu, mitandao na ushiriki wa maarifa na harakati za wanawake na wasichana.
- Muda wa utekelezaji wa mradi unaopata ruzuku kwa kupitia dirisha hili unapaswa kuwa kati ya miezi 6 na mwaka 1
- Mradi utakaopata ruzuku kwa kupitia dirisha hili uonyeshe kwa uchambuzi wa jinsi lengo/malengo yatakavyo polekea kuwezesha walengwa, hasa wale waliotengwa au makundi maalumu la kutoa sauti kwa wanawake waliotengwa kama ilivyoainishwa kwenye wito wa ombi.
- Dirisha hili liko wazi kwa mashirika ya wanawake, wasichana na watoto katika ngazi za taifa na za jamii ambazo zinahitaji ruzuku za kuimarisha mashirika au kujenga mbinu za kimkakati za kuendeleza harakati za walengwa wao, ikiwemo kujenga nguvu za pamoja.

**3. DIRISHA LA UFADHILI LA KIMKAKATI**

Chini ya dirisha hili, tunatafuta kuwekeza na kushirikiana na Asasi, Mitandao na majukwaa katika ngazi ya taifa na jamii, yanayotetea haki za wanawake, wasichana na watoto na ambayo yana uwezo wa ujenzi wa harakati-jumuishi zinazofikia wadau /makundi mengi katika sekta nyingi wakiwa na lengo ya kukuza mwingiliano kati ya agenda ya wanawake, wasichana na watoto katika sekta nyingine ili kuimarisha mikakati ya ujenzi wa harakati za wanawake katika sekta zote na hivyo kukuza nguvu za pamoja/tapo katika maeneo mbalimbali. Muda wa utekelezaji wa mradi unaopata ruzuku kwa kupitia dirisha hili unapaswa kuwa kati ya mwaka 1 na miaka 2.

Katika muundo huu, tunakubali mapendekezo ya miradi ambayo yanalenga kuanzishwa au kuongeza kasi ya hatua ambazo zinakuza vitendo vya pamoja vya utetezi, majukwaa jumuishi, Mitandao ya kukuza ujuzi wa uandishi, mitandao na kujifunza katika sekta mbali mbali za wanawake, wasichana na watoto nchini.

**VIGEZO VIKUU VINAVYOANGALIWA KATIKA UTOAJI WA RUZUKU**

Waombaji wanapaswa kujitahidi kuzingatia vigezo vifuatavyo wakati wa kuandaa andiko la mradi

**1. KUOANA KWA MALENGO YA MRADI NA MAHITAJI MAKUU YA KIJINSIA KATIKA JAMII**

- Andiko ambalo linaonyesha jinsi malengo yatakavyokidhi matamanio ya wadau katika kuchangia juhudi za kuleta usawa wa kijinsia na ukombozi wa fikra katika maeneo yaliyoainishwa kutekelezwa na mradi

**2. UWEZO WA MTANDAO, SHIRIKA/KIKUNDI & UFAHAMU WA TATIZO LA MSINGI LA KUTATULIWA NA MRADI**

- Andiko la Mradi lenye kuhakikisha kwamba kuna uchambuzi wa kina kuhusu uwiano kati ya tatizo la kutatuliwa na mikakati iliyowekwa na matokeo tarajiwa yanayopimika.
- Andiko la Mradi linalo onyeshe uwezo madhubuti wa Mtandao, Taasisi, Shirika, au Kikundi husika kwenye kutekeleza mradi pendekezwa.
- Andiko la mradi linalo akisi ushiriki mpana wa wadau katika kuibua, kutekeleza na hasa ikuhusisha wale walioathirika kwa kiasi kikubwa na tatizo linalotakiwa kutatuliwa.
- Andiko la mradi linalo akisi juhudi kuelekea ujenzi wa ushirikiano na nguvu za pamoja kati ya mashirika ya haki za wanawake katika ngazi mbali mbali kwa lengo la kuunda/kuimarisha utendaji wa Mitandao na Majukwaa kwa ajili ya ukuzaji wa haki za wanawake na wasichana ili kuwaongezea uwezo wao katika Nyanja mbali mbali.
- Andiko la mradi linalo onyesha uwezo na muendelezo wa kuibua na kutunza mafanikio (na mafunzo) ambayo yanaweza kuigwa na kutumika katika mradi mingine katika ngazi mbalimbali.
- Andiko la mradi linalo onyesha ubunifu wa mikakati ya kiutekelezaji na matokeo yake.

**WAOMBAJI WA RUZUKU WAFUATE HATUA ZIFUATAZO:**

I. Kuwasilisha Andiko Fupi la Mradi (lisilozidi kurasa 12) likielezea mradi pendekezwa utakaotelezwa
II. Andiko la mradi liwe na viambatanisho vifuatavyo
- Nakala ya Cheti cha Usajili
- Nakala ya Katiba ya Shirika/Kikundi
III. Kutoa, kuomba, au kushawishiwa kwa namna yeyote kutoa au kupokea rushwa kutapelekea kuchukuliwa kwa hatua kali za kisheria.
IV. Tumia Fomu ya Muongozo wa Maombi ya Ruzuku inayopatikana katika tovutI ya WFT Trust: www.wft.or.tz.

Maombi yote ya ufadhili wa Mradi itumwe kwa anuani ya posta au barua pepe kwa anuani zilizoainishwa hapa chini.

- **Email, grants@wftrust.or.tz**
- **S.L.P 79235, Dar es salaam**
- **Ofisi za WFT TRUST Nyumba namba 17 mtaa wa Rufiji (Masaki) Dar es Salaam.**
- **Simu 0753 912 130**

**Mwisho wa Kupokea Maombi ni tarehe 28 Februari 2021**

*** TAFADHALI FAHAMU KUWA WATAKAO JULISHWA KUHUSU MAOMBI YA RUZUKU NI WALE TU AMBAO MAANDIKO YAO YA MRADI YATAPITISHWA. KAMA HUJAJULISHWA KUHUSU KUPITISHWA KWA ANDIKO LAKO IFIKAPO TAREHE 31 MACHI 2021, BASI ANDIKO HILO HALIKUCHAGULIWA NA UTAENDELEA KUSHIRIKIANA NA WOMEN FUND TANZANIA -TRUST KWA NJIA NYINGINE MBALIMBALI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ma-DC wawajibike

JUZI Rais John Magufuli, akizungumza na wananchi wa Bahi mkoani Dodoma, alisema hatasita kuwaondoa wakuu wa wilaya ambao maeneo yao yatabainika kuwa na njaa.

Aidha, alisisitiza kuwa serikali haitatoa chakula cha msaada kwa mtu yeyote, zaidi wananchi watatakiwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha wanapata chakula cha kutosha na ziada kwa ajili ya familia zao na biashara.

Hii ni mara ya pili kwa kiongozi huyu kusisitiza juu ya suala la wajibu wa Ma-DC kuhakikisha chakula kinapatikana kwa kuwa wajibu wao mkubwa ni kuhamasisha na kusimamia kwa karibu shughuli za maendeleo.

Moja ya shughuli hizo ni wananchi kushiriki shughuli za uzalishaji hususan kilimo ambacho moja kwa moja kitawawezesha kupata chakula cha kutosheleza mahitaji yao, lakini wataweza kuuza kwa ajili ya kupata kipato.

Itakumbukwa kuwa sekta ya kilimo ndiyo inayoongoza kwa kuajiri idadi kubwa ya Watanzania, hivyo ndiyo tegemeo lao kubwa.

Iwapo Mkuu wa Wilaya atakuwa mstari wa mbele kuhamasisha shughuli za maendeleo, wapo wananchi watakaofanya vizuri zaidi na kutumia vyema fursa zilizopo kuendeleza kilimo na kujipatia kipato.

Majukumu ya kuhamaisha maendeleo kwa viongozi hao yanapaswa kufanywa kila siku kwa kwenda vijijini, kuwa mfano kwa wengine kiasi cha kuwa na mashamba darasa, ambayo yatawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao.

Uwepo wa mashamba darasa ni msaada mkubwa kwa kuwa wataweza kujifunza kwa vitendo, kama ni kilimo cha mahindi au maharagwe, maana yake watajifunza zaidi na kuhamishia ujuzi huo kwenye mashamba yao.

Lakini katika wilaya kuna maofisa kilimo na ugani ambao wanawajibu wa kutembelea wananchi na kuwashauri masuala mbalimbali ya kilimo na ufugaji, ikiwa watashirikiana na DC maana yake elimu husika itawafikia wananchi wengi kwa wakati mwafaka.

Ni muhimu sana kwa viongozi hao kutimiza wajibu wao kwa kuhakikisha wana ratiba ya kuwatembelea wananchi hasa nyakati za maandalizi ya mashamba kwa ajili ya kilimo, ili watumie vyema muda huo na kuzalisha kwa wingi.


Lakini kupitia ubunifu ni muhimu kujadili masuala ya masoko ya chakula wanacholima, kwa kuwa baada ya kujitosheleza kwa chakula kinachofuata ni kuuza ziada kwa ajili ya mahitaji mengine na changamoto kubwa huwa ni kuyafikia masoko.

Ni muhimu sana ukafanyika mjadala wa namna ya kupata masoko ya mazao hayo, kwa kuwa ndiyo namna ya kupata fedha za gharama za kilimo.

Tunaamini ma-DC wamemsikia Rais Magufuli, hivyo watawajibika kuhakikisha wanasimamia maendeleo hususan kilimo ili nchi ijitosheleze kwa chakula.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Daladala Dar zinavyowapa mtihani wanafunzi wanaosoma shule kutwa

**WANAFUNZI** wengi wanaoishi maeneo ya mijini ikiwamo jijini Dar es Salaam, usafiri wao mkubwa wanaotumia ili kuwahi masomo shuleni au kurudi nyumbani, ni wa daladala.

Pamoja na kutegemea usafiri huo, wamekuwa wakikumbana na vikwazo kutoka kwa makondakta na madereva, ambavyo husababisha wachelewe kufika shule kwa wakati au kurudi nyumbani.

Miongoni mwa vikwazo hivyo, ni kukataliwa kupanda daladala na wakati mwingine kutakiwa kutoa nauli ya mtu mzima badala ya ile ambayo imeelekezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Wanafunzi wanaosoma shule za Kimara Bonyokwa jijini Dar es Salaam au wanaotoka maeneo hayo kwenda kusoma kwingine, ni mingoni mwa wanaokumbana na vikwazo hivyo, hasa vya kulipa nauli ya mtu mzima.

Kwa kawaida, mwanafunzi anatakiwa kulipa nauli ya Sh. 200 kwa ruti moja. Lakini, kwa magari ya kutoka Kimara Mwisho kwenda Bonyokwa au kutoka Bonyokwa kwenda Kimara Mwisho, hutozwa nauli ya mtu mzima. Hiyo ni mifano ya kinachojiri ndani manispaa za jiji.

Nauli hiyo ya mtu mzima katika barabara hiyo, shilingi 500, hivyo katika magari hayo, si mwanafunzi wala mtu mzima, wote wanalipa kiwango kimoja cha nauli, kinyume na maelekezo ya LATRA.

Mazingira hayo ya wanafunzi kutozwa nauli kubwa, ni mzigo kwao na hata kwa wazazi na walezi wao, ambao huwapa nauli za kwenda shule wakiamini kiwango kinachotozwa ni kile cha LATRA, kumbe sivyo.

Awali, barabara kati ya Kimara Mwisho hadi Bonyokwa haikuwa na ruti rasmi ya daladala, badala yake walikuwapo watu wachache walioweka magari yao huko zikiwamo aina ya Hoah, Hiace, taksi bubu na hata bajaji.

Zote hizo kila abiria bila pasipo kujali ni mtoto au mtu mzima, nauli ilikuwa Sh. 500 kwa kila mmoja. Ni hali iliyokuwa na madhara, wanafunzi walikaa vituoni kwa muda mrefu kusubiri usafiri ambao tozo yake angalau ililingana nauli zake.

Katika mazingira hayo, vijana hao waliishia kujikuta wanachelewa kufika shule au nyumbani.

Wapo wengine waliolazimika kutembea umbali wa kilomita hadi tatu kutoka Kimara Mwisho hadi shuleni, waliposhindwa kumudu nauli ambayo wao kwa namna moja ama nyingine hakuwa na uwezo wa kuilipa.

Kwa nauli za kawaida, mwanafunzi anatakiwa kutoka Kimara Mwisho hadi shuleni maeneo ya Bonyokwa kwa kutumia Sh.400 ambayo ni ya kwenda na kurudi, sasa wanatumia Sh. 1,000.

Tatizo hilo haliishii hapo tu, bali kuna wakati nauli imetegemea wakati au muda maalum kwa kuwa asubuhi inaweza kuwa Sh.500 kwa safari ya Kimara Mwisho hadi Bonyokwa.

Lakini, kuanzia jioni, kuna kawaida nauli kuanza kupanda. Si ajabu kukuta jioni nauli ikiwa Sh. 1,000 kwa kila abiria awe mwanafunzi au mtu mzima, kutegemea na wingi wa abiria na uhaba wa magari, hali ambayo kwa ujumla iliangukia zaidi kuwa mzigo kwa wanafunzi.

Kwa ujumla, sekta ya usafirishaji abiria hasa katika Jiji la Dar es Salaam, inakabiliwa sana na hali fulani ya soko holela lisilokuwa na mpangilio maalum na linalosababisha mzigo usio wa lazima kwa baadhi ya watu.

Usafiri wa eneo hilo umekuwa ni kila aliyeweka gari barabarani anataka kupata faida, bila ya kufuata maelekezo ya LATRA, ambayo yameweka viwango vya nauli kwa mtu mzima na mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari.

Itakumbukwa, kuna mikakati ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliyewahi kusema kuwa serikali ya mkoa ilipanga kuingiza magari 20 maalum kwa ajili ya wanafunzi. Hata hivyo, ameondoka kabla mikakati hiyo ikiwa haijatimia.

Kwa ujumla, nauli ndogo ya wanafunzi tofauti na watu wazima, ni tatizo.

# Miundombinu ya umeme treni ya kisasa yakamilika

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MIUNDOMBINU ya umeme katika treni ya kisasa ya umeme kwa kipande cha awamu ya kwanza kutoka Dar es Saalam mpaka Morogoro imekamilika kwa asilimia 100, huku Watanzania wakitakiwa kutokuwa na hofu ya kukatika kwa umeme wawapo safarini.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema hayo alipotembelea na kukagua miundombinu ya umeme katika kituo cha kupokea na kupooza umeme kilichopo Kingolwira mkoani Morogoro.

Waziri Kalemani alieleza kuridhishwa na kazi zilizofanyika hadi sasa katika mradi huo na kubainisha kwa awamu ya kwanza yenye kilometa 160 kutoka Dar es Saalam hadi Morogoro, miundombinu ya umeme tayari imekamilika kwa asilimia 100.

"Baada ya siku 18 kuanzia leo kama treni ingekuwa tayari ingeanza kutembea kutokana na kukamilika kwa kipande hicho...Tanzania inakuwa nchi ya kwanza kutembeza treni ya umeme kwa nchi za Afrika Mashariki, hivyo Watanzania wanapaswa kujivunia kwa hilo," alisema Waziri Kalemani.

Kuhusu hatari ya kukatika umeme kwa treni zinapokuwa safarini, Waziri Kalemani alisema umeme uliopo ni wa kutosha na Shirika la Umeme (TANESCO) limetenga megawati 70 kwa ajili ya kutembeza treni hiyo ya mwendo kasi, umeme utakapokuwa wa kutosha na wa uhakika.

Alibainisha kuwa mabehewa yatakayokuja yatakuwa na uwezo wa kutunza umeme kuanzia muda wa nusu saa hadi saa mbili na kwamba kama ikitokea hitilifu ya umeme treni hiyo itaendelea kutembea bila kukwama.

Meneja mwandamizi wa miradi kutoka TANESCO, Mhandisi Emanuel Manilabona, alisema wamekamilisha miundombinu yote na tayari nguzo zote 462 zimekamilika pamoja na vituo vya Pugu, Ruvu na Kidugalo.

# TAKUKURU kufuatilia mabilioni ya wadaiwa sugu wa PSSSF

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro, imeelekeza nguvu zake kufuatilia Sh. bilioni 5 .3 kutoka kwa wadaiwa sugu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumsihi wa Umma (PSSSF) ili warejeshe zitumike kwa malengo ya mfuko.

Kaimu Mkuu wa taasisi hiyo, Mkoa huo, Manyama Tungaraza, alisema katika taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu kazi zilizotekelezwa na taasisi hiyo Mkoa wa Morogoro kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Oktoba 2020 hadi Desemba 2020.

Alisema, katika kudhibiti ubadhirifu wa mali za umma, TAKUKURU itaanza kufuatilia Sh. 5,302,238,457.39 kutoka kwa wadaiwa sugu wa PSSSF ili waweze kurejesha fedha hizo mapema iwezekanavyo ili zitumike kwa malengo ya mfuko.

Alisema huo ni mkakati au maeneo ya vipaumbele kwa kipindi cha Januari - Machi, 2021.

Wadaiwa hao ni vyama vya akiba na mikopo ikiwamo TPAWU SACCOS- Kilombero, Chuo cha Sukari Saccos- Kilombero, Mzinga Saccos - Morogoro pamoja na SUA SACCOS - Morogoro.

"Lengo letu ni wadaiwa wafanye jitihada zinazotakiwa kuhakikisha fedha zote zinarudi haraka iwezekanavyo," alisema Tungaraza.

Alisema katika kuimarisha uzuiaji rushwa katika kipindi cha mwezi Oktoba 2020 hadi Desemba 2020, taasisi imeweza kuokoa Sh. 106,020,580 zilizokuwa zimefanyiwa ubadhirifu.

Alisema baada ya kukamilisha uchunguzi wake imeweza kurejesha fedha hizo kwa watu wanyonge (waathirika) waliokuwa kwenye SACCOS mbalimbali kiasi cha Sh. 25,157,000 kwa wakulima, wafanyakazi shilingi 49,742,000, wafugaji shilingi 5,700,000, Serikali shilingi 11,190,000 na mikopo umiza shilingi 14,231,580.

Tungaraza, alisema katika kipindi hicho mali zenye thamani ya Sh. milioni 12 zimeweza kuokolewa, zikiwamo pikipiki yenye namba za usajili DFPA 4345 iliyotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro mwaka 2018 kwa Ofisa Elimu Kata ya Uwanja wa Taifa, Jane Shoo, kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za uboreshaji wa elimu katika kata hiyo.



Wafanyabiashara wadogo wakiuzia biashara zao kwenye maeneo ya kuegesha magari katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam juzi, hali ambayo husababisha usumbufu kwa madereva. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wazawa sasa kuongoza migodi yote ya Barrick

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya madini ya Barrick imesema ndani ya muda mfupi ujao shughuli zote za uchimbaji wa madini na menejimenti ya migodi inayomilikiwa na kampuni hiyo, zitakuwa zikifanywa na Watanzania kwa asilimia 100.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Mark Bristow, wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari waliotembelea mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu uliopo Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga.

Alisema kwa sasa Watanzania wanaofanyakazi kwenye migodi yake ni asilimia 96, hivyo malengo waliyojiwekea kipindi kifupi kijacho ni kuhakikisha wanafika asilimia 100 ya wazawa wanaoendesha shughuli zake hapa nchini.

Alisema sera ya kampuni hiyo inayofanya kazi kwenye nchi 13 ni kuendelea kuajiri wazalendo wa nchi husika, na kwamba wamefanikiwa kuajiri wafanyakazi wapya 600 kwa mgodi wa Bulyanhulu pekee katika kipindi cha mwaka mmoja.

Bristow alisema migodi wa North Mara na Bulyanhulu ilifanya uzalishaji kwa kiwango chake cha juu kwa mwaka 2020, na kwamba migodi hiyo yote imefanyiwa maboresho na kufanya shughuli za uchimbaji kuwa bora zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Alisema baada ya maboresho yaliyofanyika mgodi wa North Mara umeonyesha matumaini makubwa kwenye uzalishaji huku uzalishaji chini ya mgodi wa Bulyanhulu ukianza upya baada ya shughuli za kuukarabati.

Bristow alisema migodi hiyo kupitia ubia na kampuni ya serikali ya Twiga ilifanikiwa kulipa gawio la Dola za Marekani milioni 250 kwa mwaka 2020, huku ikiwekeza Dola milioni 800 kwenye uchumi wa Tanzania kupitia kodi na tozo mbalimbali.

Alisema fedha hizo ni zile zilizotolewa na kampuni hiyo kupitia vibali vya wafanyakazi, kodi, ujenzi wa miundombinu, mishahara kwa wafanyakazi na malipo kwa Watanzania wanaotoa huduma mbalimbali kwenye migodi hiyo.

Alisema kufanya vizuri kwa migodi hiyo miwili kumetokana na kasi na ufanisi uliowezeshwa na timu ya kampuni hiyo ukanda wa Afrika na Mashariki ya Kati kwa kuchapa kazi licha ya changamoto ya ugonjwa wa corona.

# Serikali yafunguka chanjo ya corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, amesema kuwa kwa sasa wizara hiyo haina mpango wa kupokea chanjo ya ugonjwa wa Corona (COVID-19) inayoripotiwa kuwapo na kutumika katika mataifa mengine.

Dk. Gwajima, aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa ufafanua kwa waandishi wa habari kuhusu kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ambukiza.

Alisema kutokana na mlipuko wa pili wa ugonjwa wa corona katika mataifa jirani, amekuwa akipokea maswali mengi kutoka vyombo vya habari kuhusu matumizi ya chanjo hiyo, pamoja na njia za kujikinga.

"Naomba ifahamike kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya inazo taratibu zake za kufuata pale inapotaka kupokea bidhaa yoyote ya afya na hufanyika baada ya serikali kijiridhisha hivyo sasa ni hadi tujiridhishe na siyo vinginevyo," alieleza Dk. Gwajima.

Alisema kuhusu mbinu za kujikinga na ugonjwa huo wizara inaendelea kuwakumbusha wananchi kujielekeza kwenye elimu ambayo imekuwa ikitolewa na wataalamu wa afya.

"Hii ni pamoja na kuimarisha usafi, kujifukiza, kufanya mazoezi, kula lishe bora, kunywa maji mengi bila kusahau matumizi ya tiba asili ambazo taifa hili limejaliwa," alisema Dk. Gwajima.

Alisema wizara kwa kushirikina na Mkemia Mkuu wa Serikali na Baraza la Tiba Asili na wananchi watengenezaji wa tiba ya asili, wameshafanya usajili wa bidhaa za tiba asili.

Alisema kuwa upo ushahidi wa kutosha kuhusu watu wengi ambao wamepata nafuu na kupona magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza baada ya kutumia dawa za tiba ya asili hata kama walikuwa kwenye matibabu ya hospitali.

"Naomba wataalamu wote na wajuzi wa tiba asili wasisite kujitokeza kufuata taratibu za kuwasilisha dawa na bidhaa zao kwa mamlaka ya maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali ili zifanyiwe uchunguzi," alisisitiza.

Alisema wizara itawapa ushirikiano mkubwa wote watakajitokeza na kujiandikisha kupitia madawati ya tiba asili yaliyoko katika halmashauri na mikoa.

"Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto imedhamiria kuinua huduma za tiba ya asili," alibainisha.

Kadhalika, alisema analielekeza Baraza la Tiba Asili kutoa orodha ya dawa zote ambazo zimepita kwenye utaratibu wa kufanya uchunguzi wa kimaabara na maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali na kuonekana kuwa ni salama. "Ifahamike kuwa dawa nyingi zinazotumika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya zinatokana na miti au mimea kwa mfano dawa ya 'kwinini' inatengenezwa kutokana na mti wa mkwinini ambao hapa Tanzania unastawi maeneo ya Lushoto, Korogwe na Mufindi, "alifafanua Dk. Gwajima.

Pia alisema serikali itaendelea kuchukua tahadhari zote za ufuatiliaji wa mwenendo wa magonjwa yote kama ambavyo imekuwa ikifanya siku zote na kuelimisha wananchi juu ya hatua za kuchukua.

"Nawaelekeza waganga wakuu wa mikoa, wilaya na waganga wafawidhi na maofisa afya mazingira, kuendelea kuimarisha mifumo yote ya udhibiti na kinga ya magonjwa kwa kushirikiana na wananchi ili kudhibiti magonjwa yote ya kuambukiza na yasiyo ambukiza, " alisema Dk. Gwajima.




Wazoa taka wakiwa kazini, eneo la Makumbusho jijini Dar es Salaam jana, huku wengine wakiwa hawana vifaa vya kujikinga na taka hizo, hali ambayo inaweza kuhatarisha afya zao. **PICHA: SABATO KASIKA.**

# Serikali yawekeza kwenye utafiti kuimarisha kilimo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema katika bajeti yake ya 2021/2022, itahakisha inapunguza baadhi ya matumizi ikiwamo ununuaji wa magari pamoja na posho na kuweka kipaumbele katika utafiti na kuboresha huduma za ugani.

Imesema lengo hilo ni kuongeza tija kwenye sekta ya kilimo.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo juzi, jijini Dodoma, alipokuwa akitoa hotuba yake kwenye kufunga kikao kazi cha Wizara ya Kilimo, maofisa kilimo na wadau wa huduma za ugani nchini.

Alisema ili kuwa na kilimo chenye tija, taifa linatakiwa kuwekeza katika utafiti ili kuongeza ufanisi katika sekta hiyo.

Prof. Mkenda, alisema ili kuongeza uzalisahaji katika mazao mbalimbali utafiti, unahitajika ili kupata mbegu bora zitakazo ongeza kiwango cha mavuno.

"Katika bajeti ijayo tutahakikisha kuwa tunaweka kipaumbele katika masuala ya utafiti, hata ikibidi kupunguza baadhi ya matumizi kama vile ununuzi wa magari pamoja na posho ili kuweka kipaumbele kwenye utafiti," alieleza Prof. Mkenda.

Pia alisema utafiti utasaidia kupatikana kwa mbegu bora, ambazo zitaongeza uzalishaji na kuliondolea taifa utegemezi wa bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo nje ya nchi.

"Inasemekana kuwa asili ya zao la michikichi ni hapa Tanzania, na hili ndiyo zao linaongoza kwa kuzalishaji wa mafuta, lakini ukiangalia hivi sasa wenzetu wa Malaysia wanavuna zaidi kuliko sisi," alisema.

Alisema zao la michikichi Malaysia hekta moja wanavuna tani 10, na Tanzania ni tani 1.6.

"Kwa hali hii huwezi kushindana na watu hawa ambao wanalima kiasi sawa na wewe, lakini wanavuna zaidi, hivyo tunahitaji kufanya utafiti ili kupata mbegu bora ambazo zitaongeza uzalishaji tofauti na ilivyo sasa, " alibainisha Prof. Mkenda.

Vile vile, alisema kutokana na hali hiyo wameshirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kufanya utafiti wa mbegu za michikichi na kufanikiwa kupata yenye uwezo wa kutoa mavuno tani tano kwa hekta.

## Wateja wa M-pesa wapata gawio la bil. 3.9/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Vodacom, imetangaza gawio la jumla ya Sh. bilioni 3.9 kwa wateja wa M-Pesa zaidi ya milioni 11 ambao wametumia huduma hiyo kwa mwaka uliopita.

Malipo ya gawio hilo yanahusu kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa kampuni. Akizungumza kuhusiana na gawio hilo, Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema faida hiyo imekuwa ikilipwa kwa wateja, mawakala na washirika wa biashara wa M-Pesa ambao wanapokea malipo kutokana na huduma au matumizi waliyofanya kupitia simu zao za mkononi.

"Huduma yetu ya pesa kupitia simu za mkononi, M-Pesa, inaendelea kuleta mafanikio ya kushangaza, ikiongeza thamani kubwa ya fedha kwa Watanzania.

Tumeona ukuaji mkubwa kwenye jukwaa la M-Pesa na wateja zaidi, mawakala, wafanyabiashara na taasisi zinazofanya biashara hadi kufikia karibu Sh. bilioni 100 kila siku," alisema Mbeteni.

Alisema Vodacom ina zaidi ya wateja milioni 11 wanaotumia huduma ya M-Pesa ikimiliki soko kwa asilimia 40, kulingana na takwimu za hivi karibuni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

"Hadi sasa kampuni hii imelipa jumla ya Sh. bilioni 143.5 ikiwa ni faida iliyolipwa tangu Julai mwaka 2015 ilipotungwa kanuni huyo na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Mbeteni aliongeza kuwa sehemu ya faida kwa kila mteja imehesabiwa kulingana na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania na itategemea, pamoja na mambo mengine, kiwango cha shughuli ambazo wateja wa M-Pesa wamefanya kwa kipindi hicho.

Alisisitiza kuwa wanaendelea kulipa faida hizo kwa wateja wao wa M-Pesa na wateja wanaweza kutuma neno AMOUNT kwenda 15300 kwa SMS ili kujua ni kiasi gani cha riba watakachopokea.

# Wadau wahamasisha taulo za kike shuleni

**Na Sabato Kasika**

WADAU wa elimu wametakiwa kuunga mkono juhudi za kuwawezesha wanafunzi kupata taulo za kike za kutosha, ili wahudhurie shule kikamilifu na kusoma kama bila kuachwa nyuma na wenzao wa kiume.

Hayo yalisemwa na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulidi, wakati akizindua ufadhili wa taulo hizo kwa wanafunzi 1,000 unaofanywa na taasisi ya Flaviana Matata Foundation.

Alisema, wadau wengine wanatakiwa kuunga mkono kile ambacho kimefanywa na taasisi hiyo, ili kuwapunguzia watoto wa kike tatizo hilo ambalo linasababisha wakose masomo kwa muda wa wiki moja.

"Taulo za kike ni muhimu kwa maudhurio yao ili kuwawezesha kusoma kikamilifu na kupata haki msingi ya elimu sawa na vijana wa kiume, hivyo wadau wote waunge mkono juhudi hizi," alisema Maulidi.

Mwanzilishi wa taasisi hiyo Taasisi ya Flaviana Matata Foundatiin, Flaviana Matata, alisema, ufadhili huo wa taulo kwa wanafunzi 1,000 ni wa mwaka mmoja na utagharimu Sh. milioni 54.

# Waharibifu wa vyanzo vya maji wapewa angalizo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, amesema serikali haitawafumbia macho watakaofanya shughuli za kilimo karibu na vyanzo vya maji ambapo sheria inakataza.

Mndeme alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa maji wa mkoa wa Ruvuma katika Manispaa ya Songea na kushirikisha wakuu wa wilaya, wabunge, meya wa Manispaa ya Songea, wenyeviti na makatibu wa CCM, makatibu tawala wilaya, wenyeviti wa halmashauri na wataalamu kutoka wilaya zote mkoani humo.

Alisema vyanzo vingi vya maji vimeharibiwa na watu wanaendesha shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo na kusababisha kuwapo kwa maji yasiyo safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

# Taasisi kusimamia usalama wa machinjio

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Mico Halal International Bureau imeleta neema mpya kwa walaji wa nyama ambapo sasa itasimamia machinjio yote nchini kuhakikisha nyama inayopatikana inakuwa salama kwa afya.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu wa taasisi hiyo, Shehe Jumanne Kasonso, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuanza kazi kwa taasisi hiyo Januari mwaka huu.

Alisema MICO imepewa kibali na Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kwa ajili ya kusimamia machinjio hayo kwa kupima nyama inayopatikana kuwa safi na salama kwa matumizi ya binadamu na kutoa vibali kwa wale wanaozisafirisha nje ya nchi.

Shehe Kasonso alisema mbali na nyama taasisi hiyo itasimamia pia viwango vya vyakula na vinywaji kuhakikisha Watanzania wanapata huduma yenye ubora wa hali ya juu na hawapati madhara kiafya.

"Sisi ni wakala wa BAKWATA, tunafanya kazi chini yake na mbali na kupima ubora wa nyama MICO inasimamia na kutoa mafunzo juu ya uchinjaji bora halali pamoja na kutoa mafunzo na ithibati kwa nyama halali zinazosafirishwa nje ya nchi," alisema.

Alitaja baadhi ya wanyama ambao taasisi hiyo imekuwa ikisimamia kuhakikisha nyama yake inakuwa na ubora na salama kwa matumizi kuwa ni mbuzi, ng'ombe, kondoo na ndege wanaoliwa.

"Mtanzania jali na ipende afya yako hivyo unapotaka huduma ya kupimiwa nyama wasiliana nasisi tuko Magomeni Mapipa jengo la Diamond Trust tutakuhudumia kuhakikisha unapata nyama ilisayo safi na isiyo na magonjwa," alisema Shehe Kasonso.

Alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanakula nyama iliyopimwa isiyo na magonjwa kama zile ambazo zimechomwa sindano za zandigana na zinginezo ambazo mnyama husika hatakiwi kuliwa ndani ya siku 30 ili kupisha dawa hiyo itoke.

"Kuna dawa ambazo mnyama akichomwa nyama yake haitakiwi kuliwa ndani ya siku 30 na maziwa yake kama anakamuliwa yasinywewe mpaka zipite siku saba sasa watu wengine wasiowaaminifu wanaweza kuyaingiza sokoni kazi yetu itakuwa kuyapima kuona kama yanafaa na kama hayafai yanatolewa," alisema.

Alisema tangu taasisi hiyo ianze kutoa huduma hiyo mwezi Januari mwaka huu mwitikio umekuwa mkubwa kwani watu mbalimbali wamekuwa wakifika kwa ajili ya kuchukua vibali kutoka MICO kwa ajili ya kusafirisha nyama hiyo nje ya nchi.




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Azania, Charles Itembe (kushoto), akiongoza wafanyakazi wa benki hiyo, kupima afya na utoaji chanjo kwa wafanyakazi wake jijini Dar es Salaam jana. Benki ya Azania imeendesha kampeni ya upimaji afya na kutoa chanjo kwa wafanyakazi wake, ili kuwalinda dhidi ya magonjwa ya homa ya ini na Ukimwi. Wengine pichani ni Meneja Rasilimali Watu Azania, Neema Masanja pamoja na wataalamu kutoka Hospitali ya Kansa ya Ocean Road, Dk. Crispin Kahesa (wapili kulia) na Abdallah Hussein ambao waliendesha zoezi hilo. . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Misitu yaiingizia halmashauri mil. 77/-

**Na Said Hamdani, LINDI**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, imekusanya Sh. 77,540,000, baada ya kuuza mazao ya misitu kutoka vijiji vitano kati ya 90 vilivyo kwenye mpango wa kuhifadhi mazingira na utunzaji wa misitu.

Ofisa Maliasili wa Halmashauri hiyo, James Elias Kabuka, ameyaeleza hayo katika mahojiano maalumu na Nipashe mjini Ruangwa.

Kabuka akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Frank Chonya, alisema mapato hayo ni malipo yaliyotokana na ada za utoaji leseni kwa wafanyabiashara waliojitokeza kwa ajili ya uvunaji wa mazao ya misitu katika kijiji hicho mwaka 2019.

Amevitaja vijiji husika vilivyo kwenye mpango wa kuhifadhi misitu ni Mchichiri, Nandenje, Ng'au, Nahanga na Mchochora, huku akitaja aina ya miti iliyovunwa na kuchana mbao ni mkongo, mvule, mpangapanga, msekese, mtondo na msufipori.

Hata hivyo, hakutaja idadi ya CBM zilizovunwa na kuuzwa kipindi cha mwaka huo 2009 kwa wafanyabiashara waliojitokeza kuvuna mazao ya misitu.

Kabuka alisema vijiji hivyo vilianza mpango wa kuhifadhi misitu mwaka 2002, baada ya wananchi kupatiwa elimu ya utunzaji mazingira na uhifadhi misitu na faida zake kupitia Mradi wa Forvac, WWF na MCDI.

Alisema kutokana na faida inayopatikana, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa ipo mbioni kuongeza wigo kuvielimisha vijiji 85 vilivyosalia kutunza na kuhifadhi misitu kupitia mashirika mbalimbali kama vile Forvac, WWF na MCDI.

# Vyumba vya madarasa vyazuia likizo watumishi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imewataka watumishi wa Halmashauri za Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama kuacha tabia ya kwenda likizo kila mwaka mwezi Novemba badala yake washirikiane kutatua kero ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Anamringi Macha, Mkuu wa Wilaya hiyo, alitoa maelekezo hayo juzi wakati akipokea mrahaba wa ushuru wa huduma (Service Levy) wa Sh. bilioni 2.387 kutoka kampuni ya uchimbaji madini ya Twiga Minerals kupitia Migodi ya Bulyanhuru na Buzwagi kwa Halmashauri ya Msalala na Manispaa ya Kahama.

"Kila inapofika Novemba yanapotoka matokeo ya darasa la saba, tumekuwa tukisubili kukumbushwa na viongozi wa ngazi za juu hasa Waziri Mkuu na Rais juu ya ujenzi wa madarasa na ununuzi wa madawati, huku tukiwa tunatambua idadi ya wanafunzi walifaulu kujiunga na kidato cha kwanza," alisema.

Aidha, alisema ufaulu wa wanafunzi kwa darasa la saba kwa Halmashauri za Wilaya ni asilimia 85 idadi ambayo imekuwa ikifahamika kila mwaka na kwamba hakuna sababu ya watumishi wa halmashauri hizo kwenda likizo badala yake washirikiane katika kutatua changamoto hiyo ambayo hujitokeza kila mwaka.

"Hatuna sababu ya kuendelea kujenga vyumba vya madarasa kwa mwendo huu wa sasa, tujipange kulingana na idadi ya wanafunzi waliohitimu elimu ya msingi, na tujenge vyumba vya madarasa kulingana na idadi ya asilimia 85 ya ufaulu wa wanafunzi kila mwaka, " alisema Macha.

Akipokea fedha hizo, Macha alishauri zilielekezwe kwa ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa ikiwamo kuboresha huduma za afya katika vituo vya afya na zahanati hasa kwa Halmashauri ya Msalala kujenga kituo cha afya katika miji mdogo wa Isaka kwenye zahanati pekee.

Awali Meneja Mkuu wa Migodi ya Bulyanhuru na Buzwagi, Benedict Busunzu, alisema, wametoa Sh. bilioni 2.3 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na Msalala ikiwa ni malipo ya ushuru wa huduma kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka jana.

Alisema, Halmashauri ya Msalala imepokea Sh. milioni 744.9 na Manispaa ya Kahama Sh. bilioni 1.642, na kwamba anatarajia kuona fedha hizo zinakwenda kukamilisha miradi ya maendeleo kwa wananchi hasa wale wanaozunguka migodi hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, alisema, kwa kiasi kikubwa fedha hizo atazielekeza katika kujenga nyumba za walimu kwa shule msingi na sekondari zilizopo kata za vijijni ili walimu wakae karibu na shule.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati), akizungumza na Ofisa Mkuu wa Biashara wa CRDB, Dk. Joseph Witts (kulia), wakati walipohudhuria kongamano la mpango kazi na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Mwanza hadi Isaka. Kushoto ni Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa wa benki hiyo, Prosper Nambaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Hospitali yakabiliana vifo vya mama, mtoto

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Kagera iliyopo Manispaa ya Bukoba, inaendelea na upanuzi wa wodi ya kinamama kujifungulia na kuongeza vyumba vya kufanyia upasuaji.

Lengo la mpango huo linaelezwa kuwa ni kupambana na vifo vya mama na mtoto.

Akizungumza na Nipashe, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Museleta Nyakiloto, alisema sababu ya kuongeza miundombinu hiyo ni ongezeko la asilimia 9 ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa robo ya mwaka kuanzia Septemba -Desemba, kutoka asilimia 8 Julai hadi Septemba.

"Kwa takwimu tulizoziona hapa na watu wanafika kupatiwa huduma kutoka kwenye vituo mbalimbali mkoani hapa, kwa robo ya mwaka kuanzia Julai hadi Septemba, hali ya vifo ilikuwa asilimia 8, lakini Septemba hadi Desemba imeongezeka na kufikia asilimia tisa," alisema Dk. Nyakiloto.

Nyakiloto alisema, baada ya kufanya ufuatiliaji wa vifo hivyo, ilibainiwa kuwa ufinyu wa chumba cha kujifungulia ikilinganishwa na rufani zinazopokelewa mama kufika hospitali akiwa na hali isiyokuwa nzuri na mtoto kuwa na utapiamlo.

"Mama anafika akiwa na hali isiyokuwa nzuri, na uchunguzi uliofanyika utaona kuwa ni damu kidogo ambayo ikimtoka anaishiwa damu na kutokana na kuchelewa kuanza kliniki, kwa kuwa akiwahi kufika kliniki anapewa ushauri wa kitaalamu kulingana na hali yake," alisema Dk. Nyakiloto.

Alisema mbali na kufanya upanuzi wa wodi, wauguzi wamepatiwa mafunzo ya miezi mitatu na kwamba hatua hiyo itasaidia kupunguza vifo vya watoto na kinamama.

## Waonywa kupeana mikono kusalimiana

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

HALMASHAURI ya Mkuranga Mkoa wa Pwani imewataka wakazi wake kupunguza kusalimiana kwa kupeana mikono ili kuendelea kuchukua tahadhari na ugonjwa wa corona.

Akitoa taarifa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichokuwa kikijadili utekelezaji wa robo ya pili ya Oktoba-Desemba 2020 hivi karibuni, Mkuu wa wilaya hiyo, Filibeto Sanga, alisema hali ya usalama kwa wilaya hiyo ni salama.

Alisema kutokana na kauli ya Rais John Magufuli hivi karibuni kuwa nchi bado iko salama kuhusiana na Covid-19, lakini kuna kila sababu ya kila mwananchi kuona haja ya kuendelea kuchukua tahadhari ili kuepukana na ugonjwa huo.

Akizungumzia kuhusiana na sekta ya elimu, aliwataka madiwani kuendelea kujitoa kwa hali na mali ili hadi kufikia Februari 28, miundombinu yote ya elimu katika wilaya hiyo iwe imemalizika.

Aidha, aliwaomba madiwani kuridhia kumaliziwa kwa majengo ya madarasa kwenye baadhi ya shule zilizopo katika wilaya hiyo.

## Wajipa miezi 6 kutatua kero ya madarasa

**Na Sabato Kasika**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara, imejipa miezi sita ya kufanya kazi ya kumaliza kero ya muda mrefu ya uhaba wa madarasa katika shule za msingi za halmashauri hiyo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Charles Magoma, ndiye aliyesema hayo wakati akizungumza na gazeti hili na kufafanua kuwa ujenzi huo ni miongoni mwa mambo waliokubaliana katika kika cha baraza la madiwani.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 2, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 12

## OFA MWAKA MZIMA...
## Mdau alipojitokeza na taulo za kike kwa wanafunzi 1000 Dar


Ukurasa 13

Watafiti TALIRI waibua mbegu mpya ‘Mbuzi Uchumi wa Kati’

ELIMU

## NA MASHAKA MGETA, HANDENI

MATUNDA ALIYOASISI DC GONDWE...

# Uhakika chakula unavyochangia kung’arisha ufaulu shule Handeni

• Yabeba umaarufu wa mkoa • vidato 5 & 6 kila tarafa zake

KUPITIA utafiti mbalimbali, lishe duni inatajwa kuwa miongoni mwa visababishi vya kushuka kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

Ikirejewa matokeo ya utafiti uliowahi kufanywa na Shirika la Chakula Duniani (WFP) na kuhusisha watoto milioni 368, ulibaini mtoto mmoja kati watano duniani wanapata chakula shuleni kila siku, katika nchi 169 zinazoendelea.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa mataifa hayo, katika nchi zinazoendelea ambako watoto wako katika hatari ya umaskini na njaa, ni asilimia 18 tu, ndio wanapata chakula kila siku shuleni, ikilinganishwa na asilimia 49 ya watoto katika nchi za kipato cha wastani.

Kwa mujibu wa utafiti huo, wanafunzi wenye njaa hawapati nguvu ya kutosha kwa ajili ya shughuli za shuleni na matokeo yake wanapatwa athari za kusinzia, kutoroka na hata kuacha masomo.

**DOKEZO LA KIMKOA**

Mnamo mwezi Februari 2, 2017, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Meck Sadiki, alikiambia Kikao Maalumu cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kwamba moja ya sababu zilizochangia mkoa huo kushuka ufaulu kwa wakati huo, ni baadhi ya wazazi kutochangia chakula cha mchana kwa wanafunzi.

Akasema, kutopatikana chakula cha mchana kwa wanafunzi, kuliwafanya washindwe kuzingatia




Wanafunzi wa wilayani Handeni, katika moja ya mikusanyiko yao. **PICHA: MTANDAO**

vyema masomo yao, katika zama takwimu zilionyesha ufaulu kushuka kwa asilimia 1.03, ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2015.

Lakini wilayani Handeni mkoani Tanga, kwenye halmashauri mbili, uhakika wa chakula unatajwa kuchangia kuipandishia ufaulu.

Katika taarifa zilizosemwa kwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Festo Dugange hivi karibuni, zinaonyesha hatua kubwa kupigwa kielimu.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, takwimu za mwaka 2019/2020 zinaonyesha wanafunzi 6,153; wavulana 2,954 na wasichana 3,199 walisajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba katika shule 118 ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni pekee.

Kati ya wanafunzi hao, 6,105; wavulana 2,939 na wasichana 3,166 (sawa na asilimia 99.21) walifanya mtihani huo huku 48 (sawa na asilimia 0.78) wakiwamo wavulana 15 na wasichana 33 hawakufanya.

Miongoni mwa wanafunzi waliofanya mtihani huo, 5,402, wavulana 2,614 na wasichana 2,788 walifaulu kuingia kidato cha kwanza 2021, wakati waliofeli walikuwa 703 (sawa na asilimia 11.42).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, William Makufwe, anasema katika miaka minne mfululizo, wamefanya vizuri kitaaluma na anasema ufaulu huo ulikuwa asilimia 62.3 kwa mwaka 2016; mwaka 2017, asilimia 73.55; asilimia 81.64 (2018), asilimia 87.7 (2019) na asilimia 88.5 mwaka jana.

Kwa Halmashauri ya Mji wa Handeni, takwimu zilizotolewa na Mkurugenzi Mtendaji, Kenneth Haule, zinaonyesha ufaulu kwa mwaka 2017 ilikuwa asilimia 78.3; mwaka 2018 ikawa asilimia 73.6, mwaka 2019 ikafikia asilimia 92.21; na asilimia 91 kwa mwaka jana.

“Hali hii imetokana na kusimamia nidhamu kwa walimu na wanafunzi...na kuendelea kutoa chakula cha mchana ambapo shule 113 kati ya 152 zilizopo wilayani humu zinatoa chakula hicho,” anasema Makufwe.

Pia kwa upande wa sekondari, taarifa hiyo inaeleza kuwa ufaulu wa kidato cha nne kwa mwaka 2019 ulikuwa asilimia 75.3 kwa halmashauri ya wilaya na asilimia 77 upande wa Handeni Mji.

**UHAKIKA CHAKULA**

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Toba Nguvila, anataja vyakula kama muhogo, mahindi, mpunga na matunda ya aina tofauti yanayostawi wilayani humo kwa wingi, ndio yanayotumika zaidi kwa chakula cha shule.

Ni hoja hiyo inaungwa mkono na Yasin Ali Mfinanga, mkulima wa matikiti maji katika kijiji cha Magamba, anayesema ustawi wa matunda hayo, ni miongoni mwa vielelezo vinavyoashiria uwapo wa vyakula vya aina nyingi wilayani kwao.

Mfinanga anasema, matikiti maji yanalimwa wakati wa mvua za vuli zinazonyesha kati ya Septemba na Novemba, zikiwa katika kiwango kidogo ikilinganishwa na masika yanayoanza ndani ya mwezi Machi na Aprili ya kila mwaka.

Anasema licha ya matunda hayo kuchochea afya za watu wakiwamo wanafunzi, yanachangia kukuza kipato cha mkulima, kwa

INAENDELEA UK.14

ELIMU
**NA SABATO KASIKA**

OFA MWAKA MZIMA...

# Mdau alipojitokeza na taulo za kike kwa wanafunzi 1000 Dar

• Mwingine ana vyumba vya kujisitiri mabinti shuleni




Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulidi, akipokea boksi la taulo za kike kutoka kwa mwanzilishi wa Taasisi ya Flaviana Matata Foundation, Flaviana Matata, kwenye uzinduzi wa ufadhili huo, wanafunzi wakishuhudia. Picha nyingine, Flaviana Matata akitoa neno kwenye hafla hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

Ni habari njema, jumla ya wanafunzi 1,000 sasa, kutoka mikoa mbalimbali nchini wanatarajia kufaidika na ufadhili wa taulo za kike, ndani ya mwaka mmoja.

Hiyo inatajwa kuwa ni sehemu ya kampeni na harakati za kitaifa zinazoendelea sasa, kuhakikisha mabinti hao hawakosi masomo wakati wanapokuwa katika hedhi.

Kimsingi ni ya ufadhili unaotokana na uhalisi kwamba, taulo za kike zina umuhimu kwa mahudhurio yao wasichana masomoni, ili wasikose mwenendo kamili wa hali inayojiri masomini, katika haki yao ya msingi ya elimu sawa kwa mabinti na wavulana.

**WALENGWA WAKUU**

Walengwa wa taulo hizo, ni mabinti wanaoishi katika mazingira magumu, wakiwamo 250 walioko jijini Dar es Salaam, ambao sasa kwa mwaka mmoja watanufaika na mahudhurio ya vipindi vyote shuleni bila kikwazo cha hedhi.

Tukio la ufadhili huo, ilizinduliwa na Ofisa Elimu wa mkoa huo, Abdul Maulidi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali, wakiwamo wanafunzi husika.

Upatikanaji wa taulo zenye ubora na salama, ni jambo litakalowawezesha wasichana kupata haki ya elimu na kuchangia malengo Namba Tatu, Nne na Tano la Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG's).

> “Tumezindua rasmi ufadhili wa elimu kwa wasichana 1,000 kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na kati yao wanafunzi 250 wanatoka Mkoa wa Dar es Salaam ambao pia watapata taulo za kike za Lavy bure.

Wakati lengo la tatu linahusu afya na ustawi bora kwa jamii, lengo namba nne ni la elimu bora, wakati inasaidia usawa wa kijinsia kufikia malengo hayo, kuwa na jamii endelevu ifikapo mwaka 2030.

Ni kwa kipindi cha mwaka mmoja sasa, Taasisi ya Flaviana Matata Foundation' imeamua kubeba jukumu la kuwasaidia taulo kwa muda wote, wasichana hao 1,000 kwa jumla ya gharama Sh. milioni 54.

Mwanzislishi wa taasisi hiyo, Flaviana Matata, amarejea mzizi wa taasisi hiyo, ni kumsomesha watoto wa kike watokao kwenye mazingira magumu.

Pia, anataja lingine ni kuhamasisha upatikanaji elimu bora katika mazingira rafiki na salama kwa wanafunzi, kupitia utoa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, ujenzi na ukarabati wa vyoo, madarasa, ofisi na nyumba za walimu.

“Tumezindua rasmi ufadhili wa elimu kwa wasichana 1,000 kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na kati yao wanafunzi 250 wanatoka Mkoa wa Dar es Salaam ambao pia watapata taulo za kike za Lavy bure,” anasema Flaviana.

Flaviana anasema, wengine 750 watapatikana kutoka mikoani na kwamba taasisi hiyo inaendelea kuwasiliana na shule mbalimbali ili kuwatambua wanafunzi walio katika mazingira magumu ili kuwafikishia taulo hizo.

Anasema, msaada huu umelenga kuhakikisha hedhi kutokua kikwazo kwa wasichana nchini wanapata elimu bora itakayowajengea misingi ya kufikia ndoto zao.

**NAFASI YA UFADHILI**

Flaviana anarejea ufadhili huo ni zao la kuchangisha pesa kupitia kampeni kuhakikisha watoto wa kike hawakosi masomo, kwa sababu ya kutomudu gharama za taulo za kike.

“Kuna watoto wengi hasa wa kike ambao wapo kwenye mazingira magumu na wanakosa haki yao ya msingi ya kupata elimu bora kutokana na changamoto walizo nazo.

Ana ushauri kuwa ufadhili huo uwe mwanzo wa kuhamasisha na kushawishi serikali, kampuni binafsi na jamii kwa ujumla, kuunga mkono juhudi hizo waweze kuwafikia na kuwasaidia wengi zaidi wenye uhitaji, ili kuinua jamii na nchi kwa ujumla.

“Inapendeza sana kuona juhudi mbalimbali zinazofanywa na watu binafsi ili kuboresha maisha ya Watanzania hasa kwenye upande wa elimu na kwa watoto wa kike,” anasema.

**REO DAR**

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulidi, aliyewakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, anawataka wadau wa elimu kuunga mkono juhudi za zinazowawezesha wasichana kupata taulo za kike za kutosha, ili wahudhurie shule kikamilifu.

Maulidi anasema, kilichoanzishwa na jambo la kuungwa mkono na wadau, ili kuwapunguzia watoto wasichana tatizo hilo ambalo linalosababisha wakose masomo kwa muda wa wiki moja.

“Flaviana unasema, wanakosa masomo kwa siku tatu, lakini ninachojua ni kwamba wengine hadi wiki moja kwa sababu ya hedhi, hivyo ninawaomba wadau wote waunge mkono juhudi zako,” anasema Ofisa Elimu Mkoa.

Anaendelea: “Taulo za kike ni muhimu kwa maudhurio yao ili kuwawezesha kusoma kikamilifu na kupata haki msingi ya elimu sawa na vijana wa kiume, hivyo nisisitize umuhimu wa wadau wote kushirikia kampeni hizi.”

Pia anasema ushirikiano kutoka mashirika ya umma, watu binafsi na taasisi kama ya Flaviana Matata, unahitajika kufanikisha afya ya hedhi shuleni na kwamba upatikanaji wake utawezesha wasichana kupata haki ya elimu.

Anasema, ili kuinua nchi, kila mtu anahusika ili iende mbele, hivyo hata kwenye suala elimu, wanafunzi wa jinsi zote kupata elimu kwa pamoja ni muhimu.

**VYUMBA VYA KUJISITIRI**

Zena Maajar Tenga, Mwakilishi wa Taasisi ya Hassan Maajar Trust (MT), inayojishughulisha na huduma mbalimbali za wanafunzi wa kike, anasema mabinti hao wanakabiliwa na matatizo mengi katika talauma.

Anasema, kwa kutambua mahitaji ya mabinti hao shuleni, taasisi yao imekuwa ikijenga vyoo na vyumba maalum vya kujisitiri katika shule mbalimbali za Dar es Salaam na Bagamoyo mkoani Pwani.

Anasema, taasisi inajulikana zaidi kwa kampeni yake ya ‘Dawati kwa Kila Mtoto’ ikiwa na makakti wa kutimiza ndoto ya kuboresha mazingira ya kusomea katika shule za msingi nchini.

ELIMU

NA RENATHA MSUNGU, KONGWA

# Watafiti TALIRI waibua mbegu mpya 'Mbuzi wa Uchumi wa Kati'

• Anazaa mapacha 3, lita 4 maziwa • Uzito wake kilo 75, sugu wa ukame

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Kituo cha Kongwa, kinafanya utafiti mbalimbali za mifugo, ikiwamo ng'ombe, mbuzi, kuku na wanyama wengine wanaofugwa ili kuiongeza thamani ya mifugo iweze kuwainua kiuchumi wafugaji.

Kutokana na utafiti huo, imeibua mbuzi jike aina ya Malya, wenye uwezo wa kuzaa mapacha mpaka watatu, lakini ana uwezo wa kuvumilia mazingira ya ukame pale anapofugwa na wafugaji katika mazingira ya aina hiyo, kulingana na sehemu husika.

Malya ni mbuzi chotara ambaye ana mchanganyiko wa aina tatu za mbuzi, zikawapa jina hilo, pia mbuzi huyo anatambulishwa kutokana na rangi alizo nazo.

Mara nyingi watu wengi wamezoea kumuita 'mbuzi mwenye madoa'. Hata hivyo, asasi ya TALIRI Kongwa wamempa jina Malya, ambalo mbuzi huyo amechanganyika na mbuzi kutoka nchi nyingine.

Hao ni mbuzi wenye vinasaba mchanganyiko aina ya dume aitwae Boer, mbegu kutoka Afrika Afrika anayesifa ya kutoa nyama na Camolai kwa ajili ya kuongeza wingi wa maziwa na mbuzi asili kutoka nchini, mwenye uwezo wa kustahimili ukame katika eneo anakofugwa.



Mbuzi wanaofugwa katika Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Kongwa, ambako kuna mbegu mpya ya mifugo hiyo iliyobuniwa. **PICHA: MTANDAO**

#### MTAFITI TALIRI

Christopher Mtwangwe, ni mtafiti kutoka Kituo cha Utafiti TALIRI Kongwa, anayefafanua kuwapo mbuzi jike aina ya Malya, anayeweza kuzaa mapacha watatu, pia maziwa wastani wa lita tatu mpaka nne anapokamuliwa mara moja kwa siku, kulingana na mazingira anayofugwa.

Mtafiti Mtwange anasema, mbuzi huyo ana faida nyingi kwa mfugaji mbuzi wa aina hiyo, kumuinua kiuchumi, akiziorodhesha mlolongo wa faida, kuwa mji pamoja na kutoa maziwa mengi, uwezo wa kuwa na kilo 60 hadi 75.

Aidha, anataja manufaa mengine ni kuongeza idadi ya mbuzi haraka, kwani matunda ya kuzaa mapacha watatu sawa na watoto wa mbuzi sita kwa mwaka na ana uwezo wa kustahimili mazingira ya ukame kama walivyo mbuzi wengine wa asili.

Mtwange anafafanua zaidi: "Huyu mbuzi ana manufaa makubwa kwa jamii ya wafugaji, kwa sababu ana sifa ambazo zitamwezesha mfugaji kuinuka."

Mtwange anafafanua zaidi ya kuwa baada ya kufanya utafiti wa mbuzi kupitia fedha ambazo zilizotolewa na serikali, kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), walibaini mchanganyiko wa mbuzi dume aina ya Boer, kutoka Afrika Kusini na mbuzi wa asili ya nchini, mwenye uwezo wa kuzaa mapacha watatu, wanaotoa maziwa na nyama nyingi.

Kutoka na sifa hizo, COSTECH ilifanya jitihada za kusambaza mbegu aina hiyo ya mbuzi jike kwa wafugaji, lengo ni kuhakikisha wafugaji wanabadilika na kufanya ufugaji wenye tija na manufaa kiuchumi.

Pia ana ufafanuzi kuwa TALIRI Kongwa hadi sasa wanahitaji kuona wafugaji wanabadilika kila siku kwa kuzingatia nchi imeshaingia katika uchumi wa kati, ili kujiongezea kipato na taifa umma kufaidika nao.

Anasema, kutokana na mchanganyiko aliyo nao mbuzi Malya, ni rahisi kwa wafugaji watakaowachukua mbuzi hao wakasaidia kuleta mabadiliko ya mifugo, pia atabadilisha biashara ya ufugaji kuwa ya kisasa.

"Tuna mikakati ya kusambaza kwa wafugaji hawa mbuzi, kwa sababu tumewafanyia utafiti na kuonekana wana uwezo wa kustahimili mazingira kama walivyo mbuzi wa asili," anasema Mtangwe.

Ana ushauri kwamba, umefika wakati wafugaji sasa wakajitokeza katika kituo hicho kupata aina hiyo ya mbuzi wenye faida kwao, akitaja mahsusi ni kwa mbuzi wenye wasifu wa hao wenye madoa.

#### BOSI COSTECH

Hadi sasa COSTECH inafanya jitihada kuhakikisha wafugaji wa maeneo hayo na nje ya wanabadilisha aina ya ufugaji, ili kufuga katika namna ya kisasa kuendana na ushindani sokoni katika biashara iliyopo.

Dk. Philibert Luhunga, Kaimu Mkurugenzi wa COSTECH, anasema hadi sasa kuna jitihada kubwa za kuhakikisha wafugaji wananufaika na elimu wanayopewa ili wapige hatua.

Anasema, ni aina ya jitihda zinazofanyika kwa pamoja zikijumuisha baadhi ya taasisi za utafiti nchini, hali inayowezesha kupatikana fedha kufanikisha hatua hizo, za utafiti jumuishi, inayowainua wakulima na wafugaji.

> Tuna mikakati ya kusambaza kwa wafugaji hawa mbuzi, kwa sababu tumewafanyia utafiti na kuonekana wana uwezo wa kustahimili mazingira kama walivyo mbuzi wa asili.

Mkurugenzi, Dk. Luhunga anasema utafiti uliofanywa na TALIRI Kongwa, umemwongezea thamani mbuzi huyo, pia inamfaidisha mfugaji kulingana na faida za mbuzi anayeelezwa.

Anasema tayari walishaanza kuwasambaza mbuzi hao katika maeneo mbalimbali waliko wafugaji, ili kuhakikisha kunashuhudiwa tija na matokeo chanya kwa wafugaji lakini kwa taifa pia.

Mratibu wa Miradi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Merchades Rutechura, anasema serikali kupitia Tume hiyo imeshatenga Sh. milioni 257 ya kufadhili miradi ya utafiti, ili kusaidia kuibua matokeo chanya kwa wakulima na wafugaji.

Rutechura anasema, mpaka sasa asilimia 70 ya fedha zilizotolewa kwa miradi hiyo, imeshatekelezwa na wanaamini watafiti wataendelea kutoa elimu ya kile walichobainii kwa wananchi, ili jamii ifugea kisasa, pia ikalima kwa namna ya kitaalamu, hali itakayowasaidia na familia zao kwa kipato cha kutosha

#### WATAFITI TALIRI

Mkurugenzi wa TALIRI Kongwa, Dk. Wilfred Munisi, anaeleza kituo hicho kinafanya jitihada za kuwaelimisha wafugaji wa maeneo hayo, ili kuhakikisha wanaikubali teknolojia hiyo itakayowapa manufaa makubwa baadaye.

"Teknolojia ya kutumia mbuzi chotara ina manufaa makubwa kwa mfugaji, kwa sababu mbuzi huyo hustahimili magonjwa mazingira ya ukame, pia hukua haraka.

"Sisi kama watafiti tutaendelea kufanya utafiti tofauti ili kuhakikisha mkulima na mfugaji wanapata elimu bora, ambayo itawasaidia kuendesha ufugaji wa kisasa na wenye tija," anasisitiza Dk. Munisi.

#### WAFUGAJI

Kutoka jamii inayozunguka eneo hilo la TALIRI, mfugaji Michael Madeje, anaanika kwamba kuanzia sasa atafuga kulingana na maelekezo ya wataalamu wa mifugo.

Ananena: "Hivi sasa taifa lipo katika Uchumi wa Kati, hivyo wafugaji wanapaswa kubadilika, ili kuendana na mazingira ya sasa ya kupiga hatua kwa kile unachokifanya."

ELIMU

# Uhakika chakula unavyochangia kung'arisha ufaulu shule Handeni



Sultan Mbuji, mkulima wa zao la muhogo akitoka shambani kwake kuvuna zao hilo, huko wilayani Handeni. **PICHA: MATANDAO**

**INATOKA UK.11**

vile gharama za uzalishaji ni ndogo hivyo kuwezesha kupata faida kubwa.

Anatoa mfano kuwa katika msimu wa 2019/2020, alivuna jumla ya tani 32 kwenye shamba la ekari saba na akapata fedha Sh. milioni 14, wakati gharama za uzalishaji zilikuwa ni takribani Sh. milioni nne.

Mkazi wa Kijiji cha Turiani katika Tarafa ya Kwamkonga, Adam Mwambea, anayejihusisha kulima muhogo kwenye shamba la ekari 200, anasema kuna haja ya kuwahusisha zaidi wajasiriamali katika sekta ya kilimo, hasa muhogo, ili wachangie ongezeko la lishe kwa wanafunzi.

Anasema wajasiriamali wengi wa kilimo biashara kama yeye, wanasafirisha mazao kama muhogo nje ya nchi China, lakini bado wana mchango mdogo kwa chakula shuleni.

"Tunazalisha chakula kingi ukiwamo muhogo, hivyo tupo tayari kuhusishwa katika mpango

> Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, taasisi za shule hazikuzalisha muhogo kama ilivyokuwa kwa wananchi waliozalisha tani 312,025 kwenye jumla ya ekari 89,150.

mkubwa wa kuwachangia chakula watoto wetu shuleni," anasema Mwambea, alipotoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya Nguvila.

Anasifu ardhi ya Handeni yenye rutuba inayostawisha mazao kwa wingi, akitoa mfano wa mche wa muhogo shambani kwake, kutoa kati ya kilo nane na 12. Mwambea anasema miongoni mwa manufaa ya kuchangia chakula ni kuwawezesha wanafunzi kubaki na kutumia muda mrefu kusoma shuleni.

"Hakuna dalili za kuwapo njaa wilayani Handeni; na uzoefu umeonyesha kuwa kuwapo kwa chakula shuleni, kumechangia kupunguza utoro na wanafunzi waliokuwa wanatoroka sasa wamerejea," anasema Mwambea.

**OFISA KILIMO**

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Chiza Kamele, anasema uzalishaji wa muhogo unaotumika kwa chakula shuleni, unahusisha wananchi na taasisi za shule.

Chiza anasema, uzalishaji wa zao hilo umekuwa ukipanda kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo, hivyo unachangia uhakika wa chakula kwa jamii, wakiwamo wanafunzi.

Anasema, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, taasisi za shule hazikuzalisha muhogo kama ilivyokuwa kwa wananchi waliozalisha tani 312,025 kwenye jumla ya ekari 89,150.

Chiza anasema, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016/2017, uongozi wa wilaya ulihamasisha kilimo cha zao hilo, hata ukasababisha taasisi za shule kuzalisha jumla ya tani 301 kwenye eneo la ekari 69.6, wakati wananchi walizalisha tani 687,245 kwa ekari 92,080.

Anaeleza mwaka 2017/2018, shule zilizalisha tani 2,825 katika ekari 382 wakati wananchi walizalisha tani 843,260 kwenye ekari 105,407.5; mwaka 2018/2019 zilizalishwa tani 4,548 kwenye ekari 568.5 (shule) na tani 2,290,332 kwa ekari 190,861 (wananchi).

Chiza anafafanua, kwamba mwaka 2019/2020, shule zilizalisha jumla ya tani 6,990 za muhogo kwenye ekari 582.5 wakati wananchi walizalisha tani 2,088,987 kwenye ekari 187,857.

"Ni kiwango kizuri cha uzalishaji chakula katika kipindi cha miaka mitano mfululizo na hivyo kuchochea uhakika wa chakula wilayani kwetu," Chiza anasema.

Musa Msindeni, mkulima katika kijiji cha Magamba, anasema licha ya changamoto zinazoikabili, sekta ya kilimo hasa katika huduma za ugani na pembejeo, uzalishaji wa mazao upo kwa kiwango kinachotosheleza mahitaji.

"Muhogo umesaidia sana kuondokana na njaa wilayani kwetu... hata wanafunzi wanachemshiwa na kula shuleni, hivyo kuwafanya wamudu vema masomo yao kwa vile hawakabiliwi na njaa," anasema Msindeni.

**HALI YA ZAMANI**

Mkazi mwingine wa kijijini, Abdallah Kibangu anasema, kuna mageuzi ya sasa wanafunzi wanabaki shuleni muda wote, tofauti na kabla ya kuwapo mpango wa chakula shuleni, wanafunzi walirejea nyumbani mchana kupata chakula na kuna amabao hakurudi tena kuendelea na masomo.

Mkuu wa Wilaya Nguvila, anasema mpango huo ulioanzishwa na mtangulizi wake, Godwin Gondwe, ni endelevu, kwa vile umechangia ufaulu mkubwa na umepokewa vyema na wakazi wa Handeni.

"Tunaendelea kuhimizana kwa wakazi wa Handeni kuhakikisha suala la chakula shuleni, linakuwa endelevu kwa ufanisi na weledi mkubwa," anasema.

Anasema uongozi unaendeleza jitihada za kukabiliana na changamoto zinazosababisha upungufu wa madarasa na madawati, pia kuanzisha shule za sekondari za juu na bwenini.

Hivi sasa wilaya hiyo ina shule za sekondari zenye kidato cha tano na sita ziko mbili pekee; Handeni na Kisaza na mpango uliopo sasa ni kufanikisha kila tarafa kuwa na sekondari ya juu. Tarafa hizo ni Chanika, Magamba, Mazingara, Kwamsisi, Mzundu, Mkumburu na Sindeni.

Katika matokeo ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2021, Wilaya ya Handeni, yenye Halmashauri ya Mji Handeni ilishinda nafasi za pili na Halmashauri ya Wilaya ya tatu kwa Mkoa wa Tanga.

***Mwandishi ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni. Anapatikana kupitia simu:+255 754 691540.***





# Zimamoto mbioni kukamilisha ujenzi wa nyumba za askari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji lipo mbioni kukamilisha ujenzi wa nyumba za askari wake katika eneo la Kikombo jijini Dodoma zitakazokuwa na uwezo wa kuchukua familia 80.

Ujenzi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni sita na zitajengwa ghorofa nane ambazo kila moja itachukua familia 10 ili kupunguza uhaba wa nyumba za askari uliopo.

Akizunguza na Nipashe, Msemaji wa Jeshi hilo, Inspekta Joseph Mwasabeja, alisema fedha hizo za ujenzi zilitolewa na Rais John Magufuli alipokuwa akizindua Makao Makuu ya Jeshi hilo jijini hapo.

"Jeshi hili bado linauhitaji wa nyumba za askari, sio Dodoma tu bali na mikoa mingine kuna uhitaji wa nyumba," alisema Inspekta Mwasabeja.

Inspekta Mwasabeja alimshukuru Rais Magufuli kuwapatia fedha hizo zilizopeleka ujenzi huo kufikia hatua nzuri, ambapo hadi sasa maghorofa sita yamefikia hatua nzuri huku mawili yapo katika hatua za msingi.

"Tunamshukuru Rais Magufuli kwa fedha ambazo alitupatia alipokuja kuzindua jengo la makao makuu tunaamini atakapokuja kuzindua atatupatia kiasi kingine cha fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi," alisema Inspekta Mwasabeja.

Alisema lengo lao ni kuona nyumba hizo zinakamilika ili kukabiliana na uhaba wa nyumba kwa askari wa jeshi hilo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Hata hivyo, alisema kwa Dodoma nyumba hizo zikikamilika zitakuwa zimepunguza uhaba wa nyumba za askari wa jeshi hilo kwa kiwango kikubwa.

Akizungumzia kuhusiana na elimu ya majanga ya kujikinga na moto kwa jamii, alisema wanaendelea kutoa elimu hiyo kwa jamii ili kuhakikisha wanakuwa na utayari wa kujikinga pale wanapoona kuna janga la moto limetokea sehemu.

"Jeshi tunajitahidi kutoa elimu hiyo kwa watu mbalimbali kwa sababu ajali haina kinga inaweza tokea wakati wowote, hivyo elimu ikitolewa jamii inajua namna ya kutoa huduma ya kwanza kabla ya jeshi hili," alisema Inspekta Mwasabeja.

# Madiwani Chamwino waitaka TANESCO kupeleka huduma

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino wamelitaka Shirika la Umeme (TANESCO) kuhakikisha linafikisha huduma ya umeme kwa wakati kwa wananchi.

Wakizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya pili ya mwaka 2021 wilayani humo, walisema kumekuwapo na ucheleweshaji wa huduma hiyo na kusababisha baadhi ya maeneo vifaa kuibiwa kutokana na kukosa ulinzi na vingine kuchakaa kabla ya kuanza kutumika.

Diwani wa Msamalo, Mussa Kaweya, alisema kuwa kuna vijiji na vitongoji ambavyo shirika hilo wametelekeza vifaa mbalimbali vikiwamo nguzo na nyaya na vimeanza kuharibika na kuibiwa na kusababisha hasara serikalini.

"Maeneo mengine wamesimika nguzo tu zimekuwa kama mapambo ya kututamanisha na hatujui hatima yake, tunaiomba TANESCO kutukamilishia suala hili muhimu kwa wakati ili wananchi waondokane na matumizi ya koroboi na kuni," alisema.

Kaweya alisema kuwa kukosekana kwa nishati hiyo kumerudisha nyuma maendeleo kwa baadhi ya taasisi, ambazo zimekosa huduma hiyo muhimu ikiwamo majengo ya serikali kama vile ya shule, vituo vya afya na nyumba za ibada na wafanyabiashara.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Keneth Yindi, alikiri kuwapo kwa baadhi ya vijiji na vitongoji havina huduma hiyo kutokana na ucheleweshaji huo.

Yindi alitaja vijiji na vitongoji ambavyo havina huduma hiyo, Chibori, Membe, Makangwa Ikongolimbe na Manda.

"Inasikitisha mno ukizingatia kuwa baadhi ya vijiji ambavyo vipo kandokando na bwawa la Mtera vimekuwa vikitoa mapato makubwa ndani ya halmashauri yetu hii ya Chamwino hivyo ninaiomba TANESCO kuliangalia hilo kama serikali inavyosisitiza umuhimu wa kuwa na umeme nchi mzima," alisema.

Naye Kaimu Meneja TANESCO Wilaya hiyo, Fatuma Makame, alisema shirika hilo hadi kufikia Desemba mwaka huu litakuwa limekamilisha uwekaji wa umeme kwa wananchi pamoja na kwenye taasisi mbalimbali.

"Taasisi zote na wale watakaoomba kuwekewa umeme hadi kufikia Desemba mwaka huu wa 2021, watakuwa wamepatiwa huduma hiyo ili kuwaondolea kero wanazozipata kutokana na kukosa umeme ambao ni muhimu kwa karne ya sasa," alisisitiza Makame.



Naibu Katibu Mkuu Jumuiya ya Wazazi (CCM) Taifa, Tija Magoma, akipanda mti eneo la shule za sekondari za Itega na Lukundo jijini Dodoma, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya sherehe za CCM kutimiza miaka 44 iliyoanza juzi nchini kote. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# NMB yavitaka VIKOBA kutumia akaunti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BENKI ya NMB imevishauri vikundi vya akiba na mikopo (VIKOBA) kutumia akaunti ya pamoja ili kujiepusha na vitendo vya uporwaji fedha za kikundi zinazokusanywa.

Meneja mauzo Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara, Ungandeka Mwakatage, alitoa kauli hiyo jana kwenye mafunzo ya vikundi vya vikoba jijini hapo.

Alisema mafunzo hayo yametolewa kwa kushirikiana na Shirika la Care International ili kuhakikisha elimu ya fedha kupitia akaunti ya pamoja ya NMB zinawafikia wateja wao.

"Tumeamua kufanya hivi kutokana na kero ambazo wanazipata hasa wanavikundi ambao kwa sehemu kubwa ndio wateja wetu, kikubwa wanakutana na tatizo la kuibiwa na wanapokuwa kwenye vikao mbalimbali namna ya kuidhinisha mikopo," alisema.

Alisema kuna wakati mtunza hazina anakuwa mbali na eneo husika huku mjasiriamali akihitaji fedha, hivyo NMB imeweka utaratibu unaosaidia kuidhinisha malipo kupitia simu ya mkononi.

"Mafunzo haya ni muhimu tutafanya maeneo yote ili kuwafikia wateja wetu ili kuwapo na usalama wa fedha zao," alisema.

Naye mwalimu wa vikundi kutoka Kata ya Makutupora, Barnabas Kiula, alisema tatizo lililopo kwenye vikundi ni uelewa kuhusu uwekaji wa akiba na urejeshaji wa mikopo.

"NMB imeleta mafunzo ya utunzaji wa fedha, usalama wa fedha zinazokusanywa, tumeelekezwa tufungue akaunti ya pamoja ili fedha hizo zisikae kwa mtu na tunapokusanya ziende kwenye akaunti ya pamoja NMB kwa usalama zaidi," alisema.

Alieleza kuwa kwa utaratibu huo wa NMB fedha inakwenda moja kwa moja mhusika na si kupewa fedha taslimu ili kuepuka kumweka hatarini na wahalifu.

Mmoja wa waliopata mafunzo, mkazi wa Mvumi wilayani Chamwino, Rehema Mabenee, alisema vikoba vimesaidia katika kusomesha watoto na kuanzisha miradi midogo ili kujikwamua kiuchumi.

"Mimi najishughulisha kulima na biashara ndogo ndogo kwa hiyo vikoba vinanisaidia sana kuna mtoto nimemsomesha hadi chuo kikuu," alisema.

# Kyela hatarini magonjwa ya mlipuko

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

WAKAZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, wanaotumia maji kutoka chanzo cha Kapapa wapo hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na kuhara.

Tishio hilo linatokana na kufanya shughuli za kilimo na ufugali katika chanzo hicho ambacho hakina uzio.

Hayo yalisemwa na Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Mlaghila, alipofanya ziara katika chanzo hicho kilichopo Halmashauri ya Busokelo Wilaya ya Rungwe.

Mlaghila alisema chanzo hicho kimeharibiwa na mifugo inayoingizwa na kusababisha uzalishaji wa maji ambao unategemewa na wakazi wa Busokelo na Kyela kutokidhi mahitaji.

"Tuna jukumu kubwa la kulinda chanzo hiki cha maji kwa sababu ndio pekee kinahudumia wananchi wa Kyela hakuna chanzo kingine cha uhakika, watu wanalima na kufuga sio sawa naomba hiyo tabia ikomeshwe," alisema Mlaghila.

Mhandisi wa maji wilayani ya Kyela, Venance Kolabigawa, alisema ili kulinda chanzo hicho lazima zitungwe sheria ndogo kutoka halmashauri ili kuwaadhibu wanaobainika kuchafua chanzo hicho.

"Tutafanya mazungumzo kati ya viongozi wa Kyela na Busokelo ili kuhakikisha tunalinda vyanzo vyetu hivi ambavyo hivi sasa vinaharibiwa na mifugo inayochungwa pamoja na shughuli za kilimo, suluhu itapatikana na itasaidia kulinda vyanzo hivi," alisema Mhandisi Kolabigawa.

Baadhi ya wananchi walisema kuwa miongoni mwa sababu zinachochangia kupeleka mifugo hiyo kwenye chanzo cha maji cha Kapapa ni eneo hilo kuwa na uoto mzuri, hivyo kufaa kwa ajili ya malisho.

Waliomba kusamehewa, na kwamba hawatarudia kufanya vitendo hivyo kwenye chanzo hicho cha maji kwa kuwa kinategemewa na wananchi weng.

Miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili wananchi wa Wilaya ya Kyela ni kukosekana kwa chanzo cha uhakika cha maji, hivyo kutegemea zaidi wilaya ya Rungwe ili kupata majisafi na salama.



Askofu Julius Laizer wa Kanisa la Naivera liliko Ungalimited, jijini Arusha, akimtambulisha mchungaji Augustina Joachim Kimaro kama Askofu Mkuu wa Kanisa la Kanaani Ministry, lililoko jijini humo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GETRUDE MPEZYA** .

# Kada CCM ataka udhibiti uvamizi vyanzo vya maji

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi CCM, Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, ameiomba Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira mkoani Mbeya, kudhibiti uvamizi wa vyanzo vya maji na uharibifu wa mazingira.

Uvamizi huo unafanywa na wakazi wa Kata ya Mwakibete, hivyo ametoa angalizo hilo ili maji yanayozalishwa kwenye chanzo cha maji cha Nzovwe kiendelee kutoa huduma na kuwafikia wananchi wengi.

Nsomba alitoa kauli hiyo jana wakati wa kupanga miti, zoezi lililondeshwa na Jumuiya ya Wazazi wa CCM Mbeya Mjini ambalo linaenda sambamba na maadhimisho ya miaka 44 ya kuzaliwa kwa CCM.

Alisema wananchi wanaozunguka hifadhi ya vyanzo vya maji hususani cha Nzovwe kuvamia mipaka na kuharibu uoto wa asili.

"Tumeamua kuazimisha miaka 44 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi CCM, kupanda miti kwenye vyanzo vya maji baada ya kuona uvamizi naomba Mamlaka ya Maji kulisimamia vizuri ikiwezakana kuzungushiwe uzio ili kuzuia uvamizi huo," alisema Nsomba.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Mkoa, James Mwampondele, aliiomba mamlaka kusimamia na kuitunza vizuri miche yote iliyopanda kwenye chanzo cha maji cha Nzovwe.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbeya, Stella Wadson, alisema zaidi ya miti 2000 imepangwa na Jumuiya ya Wazazi ya CCM Mbeya Mjini, na kwamba imepandwa maeneo yote yaliyovamiwa na makazi ya watu.

# Waonywa kuajiri watoto mashamba ya tumbaku

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

SERIKALI wilayani Chunya mkoani Mbeya, imeonya baadhi ya wakulima wa tumbaku kuacha tabia ya kuajiri watoto kwenye vibarua vya mashamba, na kwamba atayebainika atachukuliwa hatua sheria.

Wakulima hao wamekuwa wakiwatumia watoto kwa lengo la kukwepa gharama za kuwalipa watu wazima ambao hufanya kazi kwa makubaliano ya kiasi fulani cha ujira.

Sambamba na hilo, watoto wanaotumikishwa kwenye mashamba wanafanyiwa ukatili mkubwa ukiwamo wa kingono na kisaikolojia na kwamba wengi wanaotoka kwenye familia duni na yatima.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Saimon Mayeka, alisema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa kawaida wa wakulima wa tumbaku.

Mayeka alisema kuna tatizo kubwa la utumikishwaji watoto wilayani humo, na kwamba wengi wao hulipwa ujira mdogo, na kwamba sababu kubwa inayochangia ugumu wa maisha katika familia zao, hivyo hulazimika kufanya vibarua kukidhi mahitaji yao.

"Tulikwenda baadhi ya vijiji ikiwamo Mafyeko, Kambikatoto haya baadhi ya maeneo ambayo yanalima kwa wingi tumbaku na yanaajiri sana watoto, tayari tumeshaanza kuchukua hatua kudhibiti ukatili huo ambao unakinzana na sheria ya mtoto ya mwaka 2009 na makubaliano mengine ya kimataifa," alisema Mayeka.

Mkuu huyo wa Wilaya alitoa wito kwa wakulima wa tumbaku kuwa mabalozi wazuri na kama wapo wakulima wanaotumikisha watoto wadogo waache vitendo vya kuwatumikisha watoto...watoto wamekuwa wakifanyishwa kazi ngumu na kudhulumiwa fedha zao wanapofanyishwa kazi. Kwa upande wake, Kaimu Meneja Mkuu wa Chunya Tobacco Co-operative Union limited (CHUTCU LTD), Juma Nshinshi, aliwataka viongozi wa wakulima katika maeneo yao kuendelea kutoa kutoa elimu kwa wakulima dhidi ya masuala ya ajira kwa watoto kuwatumikisha kwenye shughuli za shamba.

Nshinshi alisema utumikishwaji wa watoto katika mashamba ya tumbaku hairuhusiwi katika taratibu za uzalishaji wa tumbaku kwa sababu wanunuzi wa tumbaku dunia nzima wanapinga kununua mazao yanayozalishwa kwa kutumia nguvu kazi za watoto wadogo.

"Tunaweza kukosa wote soko la tumbaku ambalo tunalo sasa endapo itabainika kuna baadhi ya wakulima wanatumikisha watoto wadogo mashambani, hivyo wanafanya vitendo hivyo waache mara moja.





# Mjasiriamali aomba uwezeshaji ufugaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKULIMA wa mboga, Muhammed Ali Suleiman, aliyeamua kugeukia kilimo cha ufugaji wa samaki wa maji baridi aina ya kambale, ameiomba serikali na wafadhili kumsaidia nyenzo za kisasa ili kuendeleza ufugaji huo.

Alisema ameamua kujiajiri na kuajiri vijana wengine katika ufugaji kutokana na gharama zilizopo kwenye kilimo cha mboga, shughuli yake ya awali.

Suleiman, aliyasema hayo jana, Kijiji cha Machui, Unguja wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mradi wa ufugaji samaki.

Alisema imani yake ni kwamba ufugaji wa samaki una maslahi zaidi kuliko kilimo cha mboga.

Suleiman, alieleza kuwa ana vifaranga vya samaki 30,000 katika mabwawa na baadhi ya vifaranga hivyo, alipewa na idara ya uvuvi.

"Nimeshauza tani 20 za samaki. Soko la samaki wa aina hii ni kubwa lakini tatizo ni uhaba wa vifaranga," alisema Suleiman.

Licha ya kujikita katika ufugaji huo, Suleiman alisema bado anahitaji elimu ya ufugaji namna ya kutumia vifaa vya kisasa na mashine ya kuzalisha vifaranga.

"Samaki nilioano sijui wana umri gani, hivyo nahitaji elimu ya ufugaji wa samaki ili kuendeleza shughuli hii niwe mfugaji wa kisasa, nikiachana na ufugaji wa mazoea," alisema Suleiman.

Kuhusu nyenzo, Suleiman alisema zitamfanya aendeleze ufugaji na kupata mafanikio ya kuufikia uchumi wa buluu na uvuvi.

Alieleza lengo lingine ni kufanya ufugaji wa kitalii, mradi ambao utatembelewa na watalii wa ndani na nje ya nchi.

Kadhalika, aliiomba serikali kumuunga mkono akitoa ajira kwa vijana kwa kuwa atachangia kuingizia kipato serikalini.

# Makamu wa Pili wa Rais ataka haki kwa yatima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameitaka jamii kuishi vyema na watoto yatima, kwa kuwapa fursa stahiki.

Aidha, aliitaka kutowanyanyapaa ili watoto hao wapate furaha kama ilivyo kwa watoto wengine.

Abdulla, aliyasema hayo katika sherehe ya ufunguzi wa tamasha la Choma Choma katika viwanja vya Fumba City Park, iliyoandaliwa na kampuni ya Dafu kwa kushirikiana na Taasisi ya Zanzibar Aids Association and Support of Orphans (ZASO children's Home).

Alieleza kwamba Zanzibar ina mahitaji mengi ambayo serikali pekee haiwezi kuyasimamia na kuyakamilisha, hivyo ni vyema jamii na watu wenye uwezo kuendelea kushirikiana na serikali.

Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, alisema kutokana na mahitaji maalum ya watoto hao, kuna haja kwa serikali kukiangalia kituo hicho kwa jicho la karibu ili kuwapatia mahitaji ya msingi watoto hao.

Zubeir alieleza kuwa, serikali ibuni mipango ya kudumu itakayowasaidia watoto kwa lengo la kupunguza mzigo katika kituo hicho na kwamba wadau watoe ushirikiano.

Mlezi wa kituo hicho, ambaye ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilisihi, Mgeni Hassan Juma, alisema lengo la kituo hicho ni kuwasaidia watoto yatima hasa walio na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Alisema kama ilivyo kwa watoto wengine, bila ya kujali hali yao, wana haki ya kuishi, kusoma na haki nyingine.



Muhammed Ali Suleiman (wapili kulia), akiwa na vijana aliowaajiri katika mradi wa ufugaji samaki aina ya kambale, akionyesha samaki anaowafuga huko Machui Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri awataka wazazi elimu ya watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, aliwataka wazazi na walezi kutoa msukumo wa elimu kwa watoto wao, ili kujenga jamii iliyoelimika iliyo na wataalamu wa fani mbalimbali.

Soraga aliyasema hayo jana katika hafla ya kuwakabidhi zawadi wanafunzi waliofaulu darasa la sita (vipawa maalum mchepuo) katika Shule ya Msingi Langoni, Wilaya ya Magharibi A, Unguja.

Alisema ili nchi isonge mbele, kuwekwe mkazo wa kuimarisha elimu ya msingi na kati ili kuwaandaa wanafunzi kufanya vyema kwenye elimu ya juu na kuzalisha wataalamu.

Kadhalika, Soraga alieleza, wazazi wakishirikiana kikamilifu na walimu, kazi hiyo itakuwa rahisi kuwahimiza wanafunzi kuzingatia masomo yao kwa kuacha mambo yanayoathiri safari yao kimasomo.

"Suala la kukuza ufaulu sio la walimu na serikali peke yao, wazazi tuna jukumu kubwa la kuhakikisha ndoto za vijana wetu na nchi yetu kuwa na wataalamu wazalendo wa kutosha linafikiwa," alisema Soraga.

Pia aliwapongeza walimu wa shule hiyo kwa jitihada wanazochukua kufikia mafanikio na kuahidi kuwa uongozi wa jimbo hilo utashirikiana na serikali, kutatua baadhi ya matatizo yanayoikabili shule hiyo.

"Tunapokusanyika hapa kuwapongeza vijana wetu hawa, tunatambua kazi kubwa mliyoifanya walimu licha ya matatizo yanayoikabili shule, hivyo nawaomba tuendelee kuchapa kazi kadri ya uwezo wetu kuhakikisha mafanikio zaidi yanapatikana," alisema Soraga.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Langoni, Said Amour Said, alisema shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 1955 hadi kufikia mwaka jana, imeongeza ufaulu hadi asilimia 98 kutoka asilimia 96 ya mwaka 2019.

Diwani wa Wadi ya Dole, Juma Wiliam Sungwa, alieleza kuwa, zawadi hizo zinawatia moyo wanafunzi watakaofanya mitihani ya mwaka huu, kufanya vizuri.

"Tumekuja na zawadi ndogo kwa mwaka huu, lakini tutatoa zawadi kubwa zaidi iwapo mtafanya vyema mwaka huu," alisema Sungwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Shule hiyo, Ibrahim Idi Said, aliwaomba wanafunzi ambao hawakufaulu katika mitihani yao kuongeza juhudi katika masomo yao.

"Mkiongeza juhudi na kuacha mchezo, mtafanikiwa na kila mmoja wenu aweke dhamira ya kufika chuo kikuu," alieleza mwenyekiti huyo.

Katika hafla hiyo, wanafunzi hao walipatiwa zawadi mbalimbali ikiwamo sare za shule, vifaa, fedha taslimu na miche ya miti ya matunda, waliyopanda katika maeneo ya shule hiyo kama kumbukumbu ya mafanikio yao.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LORDGUARD LEON MOSHA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1343-0071** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ANNE MARIE** mwaka **2017**,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/CEN/RB/605941/2020**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA KADI YA GARI

**NDUGU AHAMAD ALY** BUNGALA WA DARESALAAM ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA SLIVER** STATION WAGON YENYE NAMBA ZA USAJILI, **T486 DCB** KADI HII IMEPOTELEA WILAYANI BARIADI MKOANI SIMIYU KWA KUIDONDOSHA TAARIFA IMETOLEWA POLISI BARIADI ,NAMBA YA RIPOTI YA POLISI,SIM/BAR/RB/31598.TAREHE 11/1/202021 YEYOTE ATAKAYEIONA AIPELEKE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **MARWA MOSES MARWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T770 DJX** . Injini namba **306s750290001**,Chassis namba **wbafa520xolm51967** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
**Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/23726/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **mayanga contractors company ltd p.o.box 10795 mwanza** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T 362 CTK ASPHALT PAVER** . kwa atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi
**Kwa KUMB: MWZ/RB/246/2019.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HABARI KIMATAIFA**

## Bobi Wine ampinga Museveni kortini

**Kampala,** UGANDA

CHAMA cha Bobi Wine kimewasilisha mashtaka mahakamani kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu.

Mawakili wa kiongozi wa upinzani, Robaert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, wamewasilisha kesi katika mahakama ya juu zaidi, wakitaka Rais Museveni azuiwe kushiriki uchaguzi ujao.

Wakili wa Bobi Wine, Medard Ssegona, alipokuwa akiwasilisha kesi hiyo, alisema kuwa hawataki kumwona Museveni akishiriki tena uchaguzi, akimshutumu kupanga ghasia. Makamu Mwenyekiti wa Chama cha NUP, John Batst Nambesh, ambaye ni naibu mwenyekiti mkoa wa Mashariki, alidai wana ushahidi wa kutosha kuonyesha udaganyifu uliofanyika katika uchaguzi uliopita.

Wagombea wengine wa urais, wamejitokeza kupinga wazi matokeo ya Uchaguzi ikiwa ni pamoja na Patric Amuriat wa chama cha FDC, Jenerali Mugisha Muntu wa Chama cha ANT, Norbert Mao wa Chama DP na mgombea wa kujitegemea Jenerali Henery Tumukunde.

Waziri wa Uganda wa Teknolojia ya Mawsiliano (ICT), Judith Nabakooba, alitoa tahadhari ya kuwafunga watu wanaoeneza taarifa za uongo kuhusu kufungwa kwa shughuli nchini humo.

Waziri Nabakooba alitweet kuwa mamlaka zinatambua kuhusu mpango wa kusababisha ghasia kuanzia Februari 3 hadi 7, mwaka huu. **BBC**

## Sudan Kusini yarudisha nyuma majira yake

**Juba,** SUDAN KUSINI

JANA Sudan Kusini imerudisha nyuma muda wake kwa saa moja nyuma.

Nchi hiyo ni kati ya nchi sita zilizopo kwenye Jumuiya ya Afika Mashariki (EAC). Waziri wa Ajira, Mary Hillary Wani, alithibitisha muda mpya umeanza kufuatwa kuanzia jana saa sita usiku.

Hata hivyo muda wa kazi haujabadilika ni ule ule, kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 11 jioni.

Taarifa kutoka mjini Juba, zilisema kuwa, Rais Salva Kiir ataungana na mawaziri katika tukio hilo la kurudisha nyuma mshale wa saa kwa saa moja kama ishara ya kuthibitisha tukio hilo.

Raia wa nchi hiyo walipewa wito kuhusu suala hilo huku, vyombo vya habari vya Sudan Kusini, vikiushirikisha umma juu ya taarifa hiyo. **BBC**

# Ufaransa yatoa neno Myanmar chini ya jeshi

**Paris,** UFARANSA

SERIKALI ya Ufaransa, imewataka viongozi wa Jeshi la Myanmar, kuheshimu matokeo ya uchaguzi uliofanyika Novemba, mwaka jana, baada ya jana kufanya mapinduzi na kumkamata kiongozi wa nchi hiyo, Aung San Suu Kyi.

Jeshi la nchi hiyo, lilitangaza mwaka mmoja wa hali ya dharura, huku likimteua Mkuu wa Majeshi, Min Aung Hlaing kuchukua uongozi wa taifa hilo.

Kyi, ni kiongozi katika Chama cha National League for Democracy (NLD) yupo kizuizini pamoja na wanasiasa wengine tangu jana.

Kauli hiyo ya serikali ya Ufaransa, inakuja wakati tayari mataifa mengine, yakilaani jeshi kudhibiti Myanmar.

"Uchaguzi ulifanyika Novemba, Aung San Suu Kyi alichaguliwa na katika hali hii tunaonya kwamba kura iheshimiwe," Msemaji wa Serikali, Gabriel Attal aliimbia redio ya Ufaransa, Info.

Attal alisema Ufaransa imekuwa ikifuatilia kwa karibu tukio la Myanmar na kwamba serikali ina wasiwasi juu ya usalama wa raia wake waliopo nchini humo.

**Mtangazaji wa televisheni inayomilikiwa na jeshi, Myawaddy TV, alisema wanajeshi walitumia kipengele cha Katiba kinachoruhusu kuchukua udhibiti iwapo taifa lipo kwenye dharura.**

Magari ya polisi yalionekana jana eneo la Yangon baada ya Jeshi la Myanmar kufanya mapinduzi, Jumapili.

Mtangazaji wa televisheni inayomilikiwa na jeshi, Myawaddy TV, alisema wanajeshi walitumia kipengele cha Katiba kinachoruhusu kuchukua udhibiti iwapo taifa lipo kwenye dharura.

Mtangazaji alisema jeshi limechukua uongozi wa nchi baada ya serikali kushindwa kuchukua hatua za kasoro zilizojitokeza miongoni mwa wapigakura katika uchaguzi mkuu wa Novemba na kushindwa kuahirisha uchaguzi huo kutokana na corona.

Kyi pamoja na Rais Win Myint walizuiliwa huko Naypyidaw, juzi usiku, msemaji wa NLD, aliliambia Shirika la Habari la AFP.

Kyi, katika ujumbe wake uliochapishwa kwenye ukurasa wake wa Facebook, alitoa wito kwa umma kutokubaliana na mapinduzi hayo akisema ni udikteta wa kijeshi.

Aidha, ilibainika kiongozi huyo alliandika ujumbe huo kabla ya kuwekwa kizuizini.

Kyi (75) ni binti wa mpigania uhuru wa Myanmar, Jenerali Aung San, aliyeuawa wakati Kyi, akiwa na umri wa miaka miwili, kabla ya Myanmar haijapata uhuru wake kutoka kwa utawala wa ukoloni wa Uingereza mwaka 1948.

Kyi alikuwa kinara wa kutetea haki za binadamu na mwanaharakati aliyejitoa mhanga kukabiliana na utawala wa kimabavu, uliodumu kwa miongo kadhaa nchini Myanmar.

Mwaka 1991, alitunukiwa Tuzo ya Amani ya Nobel, huku akiwa kifungo cha nyumbani ambacho alitumikia tangu mwaka 1989 hadi 2010.

Novemba, mwaka 2015 alikiongoza Chama cha NLD, kwenye mashindano ya kwanza ya wazi ya uchaguzi tangu miaka 25 kupita.

Katiba ya Myanmar ilimkataza kuwa rais kwa sababu ana watoto ambao asili yao si nchi hiyo. **RFI/BBC**



Mkuu wa Jeshi nchini Myanmar, Min Aung Hlaing, ambaye tangu juzi usiku anaongoza nchi hiyo, baada ya jeshi kulidhibiti taifa hilo. **PICHA/REUTERS**

# Ramaphosa akiri ugumu uenyekiti AU

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amesema wadhifa wa Uenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU) ni mgumu na kufananisha kama 'kubatizwa kwa moto.

Muhula wake wa mwaka mmoja kama mwenyekiti wa AU, utamalizika wiki hii na kiti hicho kitachukuliwa na Rais wa Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi.

Ramaphosa alisema kazi yake kubwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita ilikuwa ni kuliongoza bara wakati wa kipindi cha janga la dunia la corona.

Alitaja mafanikio mengine katika upande wa kuimarisha amani, kuwawezesha wanawake kufungua biashara katika bara la Afrika.

"Katika kipindi hicho, eneo huru la biashara (AfCFTA) liliweza kuzinduliwa na kutangazwa kwa ari mpya ya biashara baina ya mataifa ya Afrika na ushirikiano wa kiuchumi," aliandika. **BBC**




# LIVERPOOL YAMSAJILI RASMI BEN DAVIES

**LIVERPOOL,** England

TAARIFA zinaeleza kuwa kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa jana usiku, Liverpool zilikubaliana na Preston kima cha pauni milioni mbili kwa ajili ya kumsajili beki, Ben Davies.

Wekundu hao walifungua mazungumzo na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza nchini Uingereza na Davies jana Jumatatu alitarajiwa kufanya vipimo vya afya.

Liverpool pia ilihusishwa na usajili wa mchezaji wa Marseille, Duje Ćleta-Car, lakini dili hilo lilishindikana kutokana na klabu hiyo inayoshiriki Ligue 1 kushindwa kupata mbadala.

Meneja wa Liverpool, Jurgen Kloop, alithibitisha kwamba atajaribu kusajili mchezaji angalau mmoja, baada ya mabeki wote wanne wa safu ya kati kupata majeraha.

Alipoulizwa juu ya nia ya timu yake kwa beki huyo baada ya Liverpool kushinda mabao 3-1 huko West Ham Jumapili, Klopp aliiambia Sky Sports: "Ben Davies, Tottenham ... sina la kusema juu yake. Kwa safu hii si shida, labda ikiwa tu kitu kingine kitatokea. "

# Solskjaer na sharti la kupunguza wachezaji

**MANCHESTER,** England

MAKAMU Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward, ameripotiwa kuwa alimwambia Ole Gunnar Solskjaer awapunguze wachezaji watatu ili kusaidia gharama za uhamisho wa beki mpya wa kati.

'Mashetani Wekundu' hao hawakuimarisha vema safu yao ya kati ya ulinzi wakati wa msimu wa uhamisho wa majira ya joto, lakini wanaonekana kuwa na mpango na Jules Kounde wa Sevilla kwa mwaka huu.

Hata hivyo, Mfaransa huyo anatarajiwa kuhitaji ada ya pauni milioni 60, na haijawa wazi namna United wanataka kushughulikia suala la ada ya uhamisho wake.

Kwa mujibu wa gazeti la Mirror, inadaiwa kwamba Woodward amemwambia Solskjaer awapunguze wachezaji watatu wasio na umuhimu mkubwa pale Old Trafford kabla ya harakati zao za kuinasa saini ya Kounde.

Taarifa zinadai kwamba Sergio Romero na Marcos Rojo wanatarajiwa kuelekea kusepa kikosini hapo, na wakati Phil Jones alikuwa anatarajiwa kuondoka kabla ya tarehe ya mwisho ya dirisha dogo jana usiku, huenda suala lake likakamilika dirisha la msimu wa joto.

Kounde inasemekana ameibuka kama lengo la kujilinda la Mashetani Wekundu' hao, lakini Real Madrid, Bayern Munich na Juventus wanaaminika pia kuwinda saini yake.






# *Aubameyang ampasua kichwa Arteta Arsenal*

**LONDON,** England

PIERRE Emerick Aubameyang, nahodha wa kikosi cha Arsenal kwa sasa bado yupo karantini na haijulikani atarejea lini uwanjani jambo ambalo linampasua kichwa Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mikel Arteta.

Raia huyo wa Gabon alitarajiwa kurejea uwanjani kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu England dhidi ya Manchester United uliokamilika kwa sare ya bila kufungana ila alikosekana ndani ya uwanja.

Auba amewekwa karantini baada ya kutoka kumjulia hali mama yake ikiwa ni njia ya kuchukua tahadhari dhidi ya janga la corona ili kujua kwamba hajapata maambukizo.

Kocha huyo amesema kuwa ni muhimu kwao kufuata utaratibu ambao umewekwa ili kutovunja sheria, hivyo wataendelea kusubiri mpaka pale atakaporejea ndani ya uwanja.

Arteta amesema kuwa: "Alikuwa amekwenda kumuona mama yake ila kwa sasa yupo karantini, hivyo tunapaswa kufuata taratibu na hatuwezi kumtumia kwa sasa."

# Silva ni mwathirika wa adhabu - Guardiola

**MANCHESTER,** England


PEP Guardiola amekiri Bernardo Silva aliathiriwa sana na adhabu ya kutoshiriki mechi msimu uliopita baada ya kudaiwa kuposti ujumbe wa kuudhi mtandaoni.

Kiungo huyo wa kati wa Manchester City, Silva alisimamishwa kwa mechi moja baada ya kumlinganisha kimzaha mwenzake Benjamin Mendy na picha ya kwenye pakiti ya chokoleti za Congo, akiamini ilikuwa ni utani tu.

Hata hivyo, suala hilo likamweka matatani na Novemba 2019, Chama cha Soka England (FA), kilikubali kuwa Silva hakukusudia utani wake kwa kutazamwa kwa jicho la kibaguzi.

Meneja wa City, Guardiola anaamini kipindi hicho cha utata kilimwathiri Silva ndani na nje ya uwanja. Lakini anaamini kuwa sasa kijana huyo wa miaka 26 ameweka suala hilo nyuma yake ili arejee kwenye kiwango kizuri.

"Ni mshindani mkubwa sana. Alicheza mchezo mzuri sana na alikuwa hodari kabisa. Kilikuwa kipindi kigumu kwake alipokuwa akishtumiwa kwa kitu ambacho hakumaanisha kilivyotafsiriwa, na hii ilimuumiza sana," alisema Guardiola.







# MESSI APIGA BAO LAKE LA 650 BARCA

**BARCELONA,** Hipania

LIONEL Messi amefikisha jumla ya mabao 650 akiwa na timu ya Barcelona. Hii ni baada ya kupachika bao katika mchezo dhidi ya Athletic Bilbao juzi.

Messi alipachika bao maridadi kupitia mpira wa adhabu katika dakika ya 20 ya mchezo huo, licha ya Athletic kujipanga vizuri kwenye ukuta wao.

Mshambuliaji huyo rai wa Argentina, alipachika bao hilo maridadi ikiwa ni lake la 49 kufunga kwa mipira ya adhabu ndogo akiwa na Barca.

Licha ya Jordi Alba kujifunga na kusawazisha matokeo, Antoine Griezmann, alipachika bao la ushindi dakika ya 74 na sasa wamewazidi Real Madrid kwa tofauti ya mabao kwenye msimamo wa LaLiga.

Barca na Madrid wote wamezidiwa pointi 10 na vinara Atletico Madrid ambao bado wanamchezo mmoja pungufu ya miamba hiyo ya soka la Hispania.

# Tuchel aanza na nyota

**LONDON,** England

CHELSEA walipata ushindi wao wa kwanza chini ya bosi mpya Thomas Tuchel walipowachapa Burnley 2-0 huko Stamford Bridge Jumapili.

Cesar Azpilicueta alianza kufunga bao kwenye kipindi cha kwanza, kabla ya Marcos Alonso, kumpatia Mjerumani huyo ushindi wake wa kwanza kama meneja wa 'Blues'.

Chelsea ilisajili hati safi ya pili mfululizo chini ya Tuchel, ambaye mchezo wake wa kwanza dhidi ya Wolverhampton Wanderers Jumatano iliyopita alisajili hati safi kwanza.

Tuchel alikuwa meneja wa kwanza wa Chelsea kupata hati safi katika mechi zote mbili za kwanza za Ligi Kuu tangu bosi wa zamani, Rafael Benitez mwaka 2012.

Blues pia ilishinda mechi yao ya kwanza ya ligi huko Stamford Bridge kwa mwaka 2021 baada ya kumaliza mechi tatu mfululizo bila ushindi, ikifungwa na Manchester City na kutoka sare na Aston Villa kabla ya mechi dhidi ya Wolves.

Chelsea sasa wanaelekeza jitihada zao kwenye mechi yao ijayo ya ligi ambapo watasafiri kuwafuata wapinzani wao, Tottenham Hotspur Alhamisi wiki hii.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR SASA ATHIBITISHA KUENDELEA KUBAKI PSG

●●● Nimebadilika, nina furaha sana hapa, nataka kukaa Paris, ninatumaini na Mbappe atasalia pia...

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Brazil, Neymar amethibitisha kuwa angependa kuongeza mkataba wake na kukaa na mabingwa wa Ufaransa, Paris Saint-Germain na anatumai Kylian Mbappe atafanya vivyo hivyo.

Neymar amekuwa akihusishwa sana na kurejea kwa awamu nyingine pale Barcelona kuungana tena na Lionel Messi, lakini sasa inaonekana hana mpango huo huku mshambuliaji huyo wa Argentina naye akiwa hajasaini mkataba mpya hadi sasa wa kubakia Nou Camp wakati huu ule wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu.

**Mbrazil huyo amekuwa kwenye mazungumzo na klabu hiyo kwa muda sasa juu ya kuongezewa mkataba wake ambao unatarajiwa kumalizika mwakani.**

Licha ya panda shuka kadhaa akiwa na PSG, pamoja na kuomba uhamisho mwaka 2019 na mashabiki wakimtaka aondoke, Neymar anatarajia kuweka nyuma hayo yote na kustawi chini ya meneja mpya Mauricio Pochettino akiwa pamoja na rafiki yake, Mbappe.

"Lakini leo, ninajisikia vizuri. Nimebadilika. Ninahisi utulivu na nina furaha sana hapa. Nataka kukaa PSG, na natumaini na Kylian atasalia hapa pia. Kwa kweli, hiyo ndiyo hamu ya kila mwana PSG."

"Tunataka PSG kuwa timu nzuri, na ninataka kuendelea kufanya kile nilichofanya kila siku huko Paris - kucheza mpira na kuwa na furaha. Hilo ni jambo la muhimu zaidi," alisema Neymar akinukuliwa na ESPN.

Wakati huo Mbappe yeye ameshaweka wazi kuwa anahitaji muda kidogo kuamua hatima yake na PSG, hivyo hataweza kusaini mkataba mpya mapema hadi awe na uhakika wa kuwapo hapo muda mrefu. Huenda kufuatia nia ya Neymar kutaka kusalia na ukaribu wa wawili hawa basi Mbappe akabadili mtazamo.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO AMTAKA RAMOS

ALIYEKUWA kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino, anataka kumchukua mlinzi wa Hispania na Real Madrid, Sergio Ramos, 34, na kumpeleka Paris St-Germain. ***(Independent)***

### UPAMECANO NJIA PANDA

MLINZI wa kati wa RB Leipzig na Ufaransa, Dayot Upamecano, 22, huenda akajiunga na Ligi Kuu England mwaka huu, huku wakala wake akisema kuwa hivi karibuni atachagua kati ya klabu mbili za Uingereza zilizo "juu" na Bayern Munich ***(Mail)***

### MBAPPE AMVUTA NDOMBELE

KIUNGO wa kati wa Tottenham, Tanguy Ndombele, 24, amesema mchezaji mwenzake wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, amejaribu kumshawishi ajiunge naye Paris St-Germain. ***(Goal)***

### LEICESTER KUMSAJILI CHALOBAH

LEICESTER City ilionyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Watford na England, Nathaniel Chalobah, 26, kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa jana usiku. ***(Leicester Mercury)***

### LIVERPOOL YAMTAKA CAR

LIVERPOOL imefanya mazungumzo na beki wa Marseille pamoja na Croatia, Duje Caleta Car, 24. ***(Mail)***

### LEICESTER NA MAITLAND-NILES

KATIKA hatua za mwisho kabla ya dirisha la usajili kufungwa jana usiku, Leicester iliamua kuweka mipango ya kumchukua kwa mkopo mlinzi na kiungo wa kati wa Arsenal na England, Ainsley Maitland-Niles, 23. Wakati huo huo Southampton, West Brom na Newcastle nazo zikimwania mchezaji huyo. ***(Mirror)***

### ERIKSEN SASA KUBAKI INTER

KIUNGO wa kati wa Denmark, Christian Eriksen, 28, ambaye amehusishwa na kurejea Tottenham, huenda akasalia Inter Milan hata baada ya siku ya mwisho ya uhamisho jana usiku, na kuwa na jukumu muhimu sana katika timu hiyo, alisema Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo ya Italia, Giuseppe Marotta. ***(Sky Sports)***

### BROM KUSAJILI WAWILI

KLABU ya West Brom inataka kusajili wachezaji wawili siku ya mwisho ya uhamisho na inamkodolea macho mlinzi Okay Yokuslu, 26, raia wa Uturuki kutoka Celta Vigo na beki wa kulia wa Uingereza, Japhet Tanganga, 21, kutoka Tottenham. ***(Express and Star)***

### HIBERNIAN ATAKUWA ENGLAND

KLABU ya Birmingham City imetenga dau la pauni milioni tatu kumsaka mshambuliaji Kevin Nisbet raia wa Scotland na klabu ya Hibernian. ***(Scottish Sun)***

### KING KUTUA BURNLEY

BURNLEY ilikuwa kwenye mkakati kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth, Josh King, 29, kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa jana usiku, suala la mshahara ndio lilikuwa kikwazo. ***(Lancashire Telegraph)***

## Cameroon vs Morocco, Mali vs Guinea CHAN

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi, Morocco, watashuka dimbani kesho dhidi ya wenyeji Cameroon katika mechi ya Nusu Fainali ya pili ya michuano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) 2021 itakayopigwa saa 4:00 usiku ikiwa ni baada ya Mali na Guinea kucheza nusu fainali ya kwanza majira ya saa 12:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

Nusu fainali ya kwanza kati ya Mali na Guinea itachezwa katika Uwanja wa Omnisport jijini Douala wakati ya pili kati ya Camerron na Morocco ikipigwa Uwanja wa Limbe.

Morocco imetinga hatua hiyo baada ya kuitoa Zambia juzi kwa kuichapa mabao 3-1 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Reunification jijini Douala, mabao yake yakifungwa na Soufiane Rahimi dakika ya kwanza, Mohammed Ali Bemammer dakika ya nane na Ayoub El Kaabi kwa penalti dakika ya 39.

Bao pekee la Zambia inayofundishwa na kocha Mserbia, Milutin Sredojevic 'Micho' lilifungwa na Moses Phiri dakika ya 80. Kwa upande Guinea, shukrani ni kwa Morlaye Sylla aliyeipeleka nusu fainali kwa bao lake la dakika ya 60 lililoipa ushinda wa 1-0 dhidi ya Rwanda katika mchezo mwingine wa robo fainali uliopigwa Uwanja wa Limbe.

## ZBL yageukia viwanja vibovu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Kuu Zanzibar (ZBL), imezitaka klabu za Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja zinazotumia viwanja vya nje ya mji (mikoani) kuhakikisha zinafuata makubaliano waliokubaliana.

Hayo yameelezwa katika kikao cha pamoja kilichowashirikisha viongozi wa timu tatu za daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ambao wanatumia viwanja hivyo.

Akizungumza katika kikao hicho juzi, Makamu Mwenyekiti wa bodi hiyo, Sheha Mohammed, alisema bado viwanja hivyo kuna mambo hayajawa sawa licha ya bodi kuruhusu kuendelea kuchezwa ligi hiyo.

Alitaja baadhi ya kasoro zilizopo katika viwanja hivyo kuwa nyasi ndefu ambazo zinatakiwa kufyekwa katika kiwango ambacho kinakubalika kisoka, kuweka alama ambazo zitatenganisha uwanja na sehemu ya mashabiki pamoja na kuweka nyavu nyeupe katika milingoti ya magoli.

# AZAM KUJIPIMA UBAVU KWA TP MAZEMBE LEO

**Na Adam Fungamwango**

AZAM FC leo itaikaribisha TP Mazembe ya DR Congo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam majira ya saa moja usiku katika mechi ya kirafiki ya kimataifa.

**Ni mechi iliyoandaliwa baada ya wenyeji kuwaomba wageni hao ambao wapo nchini kwa mwaliko wa Klabu ya Simba kwenye michuano ya Simba Super Cup ambayo ilimalizika Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa Wekundu wa Msimbazi hao kutwaa kombe.**

Wakati TP Mazembe ikizidi kupata mechi za kujiandaa na Ligi ya Mabingwa Afrika ngazi ya makundi, Azam inajiandaa dhidi ya Simba kwenye mechi ya kiporo cha Ligi Kuu Tanzania Bara itakayopigwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa, mechi hiyo itakuwa kipimo kizuri kwa timu yao si kwenye mechi dhidi ya Simba tu, bali michezo yote ya Ligi Kuu kwa jumla na kuwa ni kipimo kizuri kwa Kocha Mkuu, George Lwandamina kuangalia vijana wake kama kutakuwa na upungufu au la.

Hata hivyo, alisema kwenye mechi hiyo, huenda wakawakosa wachezaji watatu ambao ni Frank Domayo, Aggrey Morris na Salum Aboubakar 'Sure Boy' ambao ni majeruhi.

"Domayo hajaanza mazoezi, lakini wachezaji waliobaki wameshaanza mazoezi kwa hiyo ni suala ya kuangalia kama wanaweza kuwa fiti kabla ya mechi," alisema.

Azam inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 32 kwa mechi 17 ilizocheza, wakati TP Mazembe inakamata nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ya DR Congo, ikiwa na pointi 32 kwa mechi 14 ilizocheza.

Katika michuano ya Simba Super Cup, TP Mazembe iliburuza mkia baada ya kuambulia pointi moja kutokana na kukubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan kabla ya kutoka sare tasa na wenyeji, Simba waliomaliza na pointi nne na kutwaa kombe hilo.

**KAZI KAZI...**



Winga wa Simba, Luis Miquissone, akimiliki mpira, huku akizongwa na beki wa kushoto wa TP Mazembe, Mganda Joseph Ochaya katika mchezo wa Simba Super Cup uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi, mechi hiyo ilimalizika kwa sare tasa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Simba yatoa sababu kocha kutosajili*

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umeweka wazi kuwa utaratibu wao mpya wa usajili hautoi nafasi kwa kocha kuwa mtu wa mwisho kutoa maamuzi ya usajili kutokana na 'janja janja' ya baadhi ya mawakala.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Crescentius Magori, ambaye mshauri wa masuala ya michezo wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed "Mo" Dewji, alisema Simba wameweka utaratibu wa usajili ambao kocha anakuwa mjumbe tu kwenye kamati ya usajili, lakini hana maamuzi ya mwisho ya usajili.

"Unajua soka sasa hivi limebadilika sana, sisi Simba tumeweka utaratibu wetu ambapo kocha si mtu wa mwisho wa usajili na tuna sababu zetu," alisema Magori.

Aliongezea kusema: "Soka sasa hivi ni biashara, mawakala wanaokuwa na makocha ndio hao hao pia wanakuwa na wachezaji, ukimpa nafasi ya mwisho kocha kusajili anaweza akaleta wachezaji anaotoka nao kwa wakala mmoja na wasiwe na ubora ila tu wanataka kufanya biashara, bahati mbaya sana makocha hawakai sana na timu anaweza akaleta wachezaji tukampa mkataba wa miaka miwili kumbe hana uwezo na baadaye kocha anaondoka anatuachia mzigo wa wachezaji wasiokuwa na msaada, sisi Simba tumeligundua hili na ndio maana tuna utaratibu wetu kwenye usajili".

Alisema miaka ya nyuma kuna timu zilijikuta zikiwa na wachezaji ambao hawakuwa na uwezo, lakini walisajili kwa shinikizo la makocha ili kufanya biashara za mawakala wao.

# Michezo

Jumanne Februari 2, 2021

Nipashe


HABARI UK.23



## Ni Cameroon vs Morocco, Mali vs Guinea CHAN

# Yanga yafunguka kumpa Fiston jezi ya Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU mshambuliaji mpya wa Klabu ya Yanga, Mrundi Fiston Abdoulrazak, akiwa ameanza kukiwasha mazoezini akiwa amevaa jezi namba saba iliyokuwa ikivaliwa na Balama Mapinduzi na kuzua sintofahamu kuhusu mustakabali wa baadaye wa winga huyo mzawa ndani ya timu hiyo, uongozi wa klabu hiyo umefunguka kwa kueleza "hakuna tatizo".

Fiston ambaye alitua nchini Ijumaa iliyopita kabla ya kesho yake kuanza mazoezi na wenzake katika kambi ya timu hiyo iliyopo Kigamboni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, tayari ameanza kuonyesha cheche zake za kucheka na nyavu mazoezini akiwa amevaa uzi namba saba ya Mapinduzi ambaye ni majeruhi kwa sasa.

Kitendo cha Fiston kupewa jezi hiyo, kumezua minong'ono mingi kwa baadhi ya mashabiki wa timu hiyo, wakijiuliza huenda tayari Yanga imeachana na Mapinduzi ambaye ameripotiwa kuendelea vizuri.

Lakini Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Fredrick Mwakalebela, alipotafutwa na Nipashe kujua kulikoni jezi ya winga huyo inakabidhiwa kwa mchezaji mwingine katikati ya msimu huku wakiwa hawajatangaza kuachana naye, alisema hakuna tatizo na atakapokuwa fiti kurejea dimbani atapewa jezi nyingine.

"Kwanza Balama anaendelea vizuri na karibuni atarejea uwanjani kucheza, kwa uhakika kabisa atacheza msimu huu, maana kwa sasa anauguza tu kidonda.

"Kuhusu jezi hakuna tatizo, akirudi atapewa nyingine, tatizo ni kwamba watu wanataka kulikuza suala hili na kuonekana ni kubwa sana, hamna shida kabisa," alisema Mwakalebela.

Alipoulizwa endapo, Mapinduzi ameridhia kuhusu Fiston kupewa jezi yake, alisema kwa kifupi "hata yeye anajua", huku akisisitiza kuwa mchezaji huyo hana muda mrefu kabla ya kurejea dimbani msimu huu.

**KAMATA HUYO...**



Msitu wa wachezaji wa TP Mazembe, wakijipanga kumdhibiti kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama (kushoto) kwenye mechi ya michuano ya Simba Super Cup iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# GOMES AGEUKIA VIPORO

## ●●● Asema amepata pakuanzia Ligi Kuu na kwa AS Vita, Tresor Mputu aitabiria Simba makubwa Ligi Mabingwa, aeleza ...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushinda mechi moja na sare moja kwenye michuano ya Simba Super Cup na kutwaa kombe hilo, Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, amesema sasa amepata mwanga na kujua wapi pakuanzia, lakini kabla ya kucheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika akili na nguvu zake anazielekeza kwanza katika kuzitafuta pointi sita za mechi mbili za viporo vya Ligi Kuu Bara dhidi ya Dodoma Jiji na Azam FC.

Katika michuano ya Simba Super Cup ambayo ilikuwa maalum kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini kumsaidia kocha huyo aliyejiunga na timu hiyo wiki mbili zilizopita kuwajua vema wachezaji wake, Simba iliichapa Al Hilal ya Sudan mabao 4-1 kabla ya juzi kutoka sare tasa na TP Mazembe ya DR Congo.

Ligi Kuu Bara mzunguko wa pili utarejea rasmi Februari 13, lakini Simba na Namungo zitacheza kwanza viporo vyao Februari 4 na 7, mwaka huu, katika viwanja tofauti.

Simba itashuka katika Uwanja wa Jamhuri Alhamisi wiki hii kuvaana na wenyeji, Dodoma Jiji FC wakati siku hiyo KMC FC ikiikaribisha Namungo FC kwenye Dimba la Uhuru jijini Dar es Salaam.

Siku tatu baadaye, Februari 7, Simba itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuikaribisha Azam FC, huku Namungo ambayo inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, siku hiyo ikiwa mwenyeji wa Ruvu Shooting katika Dimba la Majaliwa mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gomes alisema mechi dhidi ya TP Mazembe imemsaidia kufanya maandalizi mazuri zaidi kabla ya kwenda kuwavaa AS Vita nchini DR Congo, lakini kwa ajili ya mechi mbili za viporo.

"Dhidi ya TP Mazembe ilikuwa mechi ngumu sana, lakini kwetu imetusaidia kupata maandalizi mazuri, kwa sababu kabla ya kwenda kucheza na AS Vita mchezo wa Ligi ya Mabingwa, lazima tushinde hizi mechi mbili za ligi ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye mbio za ubingwa," alisema Gomes.

Alisema wachezaji wake walicheza vizuri mechi dhidi ya TP Mazembe na kukosa nafasi nyingi jambo ambalo anaamini haikuwa bahati kwao.

"Jambo zuri hatujafungwa ni mwanzo wa kujifunza na kuona upungufu wa kikosi, wachezaji wamefanya vizuri wanastahili pongezi, nina imani tutazidi kuimarika kwenye mechi zijazo," alisema Gomes.

Kwa upande wa straika wa mkongwe wa TP Mazembe, Tresor Mputu, akizungumzia mchezo huo wa Super Cup, amekimwagia sifa kikosi cha Simba na kusema kama wachezaji wa timu hiyo wanaweka nidhamu na bidii, mwaka huu na hata mwakani kitafika mbali sana kwenye michuano ya kimataifa, hasa Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ilikuwa ni mechi nzuri, siku zote naijua Simba ni timu nzuri. Tumeshawahi kucheza nayo mara kadhaa na kila tunapocheza mechi inakuwa ngumu na ninachofurahi ni kuona wameweza kuendelea kutengeneza kikosi kizuri. Mara hii kimeongezeka kidogo uimara na nina uhakika kama wachezaji wakiweka nidhamu, bidii na kujituma, basi wanaweza kufika mbali," alisema Mputu, mmoja wa wachezaji wenye heshima kubwa si kwenye klabu ya TP Mazembe tu, bali nchi nzima ya DR Congo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042